**RIPOTI MAALUM- 2**
Kibong'oto yaanika ukubwa tatizo kifua kikuu kwenye migodi
UKURASA 4

**CHADEMA**
yatuma salamu za uchaguzi 2025 Zanzibar
UKURASA 5

**MAISHA YALIVYO**
Zijue dalili za hatima ya mtoto iliyopindishwa
UKURASA 11


# Nipashe JUMAPILI
MWANGA WA JAMII
Jumapili Oktoba 6, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0581821
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




**SLOT ATAFUTA NAFASI KWA NUNEZ**
UKURASA 22



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Muliro Jumanne Muliro

# Polisi yaonya kutumia jina lake kufanya uovu

**YASEMA** wamo watuhumiwa utekaji, mauaji, yataka mamlaka za uchunguzi kuheshimiwa...
*Endelea ukurasa 3*



Makamu Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji Rufani mstaafu Mbarouk Salim Mbarouk (kushoto), akimsikiliza Ofisa wa Tume kutoka Idara ya TEHAMA na Daftari, Lazaro Madembwe, wakati alipotembelea kituo cha mafunzo ya waandishi wasaidizi na waendesha vifaa vya bayometriki, katika Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba jana. Mafunzo hayo ni maandalizi ya mzunguko wa sita wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura, utakaojumuisha mikoa mitano ya Zanzibar na unatarajiwa kuanza Oktoba 07 hadi Oktoba 13, mwaka huu. **PICHA: INEC**

**RIPOTI MAALUM**
## Wahitimu la saba wanavyobeba jukumu la wazazi kusaka fedha
UKURASA 2

## Hungary yakunwa Tanzania usimamizi kwa sera za fedha, uchumi
UKURASA 3

**MICHEZO** **FADLU: HATUNA WA KUMLAUMU** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

RIPOTI MAALUM



Mhitimu wa darasa la saba, Melison Samwel akichota maji katika moja ya visima, wilayani Magu, mkoani Mwanza, kwa ajili ya kwenda kuyauza katika migahawa na makazi ya watu. Hununua madumu tisa kwa bei ya 300/- na kuyauza kwa 2,000/. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Wahitimu la saba wanavyobeba jukumu la wazazi kusaka fedha

**Na Waandishi Wetu**

NI hatua mojawapo ya safari ya maisha katika elimu. Safari hiyo ni kuhitimu elimu ya msingi na kuanza maandalizi ya kuanza elimu ya sekondari. Kufikia hatua hiyo ni mafanikio na furaha kwa mwanafunzi na wazazi.

Lakini kwa kufikia hatua hiyo na kusubiri ifikapo Januari, mwakani, kuanza elimu ya sekondari mtoto anafanya nini? Hilo ni fumbo kubwa na wajuao ni wale wanaomzunguka.

Wakati hali ikiwa hivyo, siku kadhaa baada ya wanafunzi hao kumaliza mitihani yao, katika maeneo kadhaa ya Kanda ya Ziwa, wamerejea nyumbani na kuanza shughuli mbalimbali za kusaka fedha. Lengo ni kutafuta fedha kwa ajili ya maandalizi ya masomo ya sekondari.

Hatua hiyo imeelezwa kuwa sehemu ya kukwamisha ndoto za watoto hao kutokana na kukosa muda wa kujiendeleza na masomo ya utangulizi ya kidato cha kwanza (pre form one) na kuishia mitaani wakiuza mboga, matunda na kufanya shughuli za kuuza dukani na ajira za muda.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, baadhi ya wahitimu wanaofanya biashara mbalimbali, wamesema badala ya kusoma masomo ya awali ya kujiandaa kwenda kidato cha kwanza inawalazimu kufanya biashara ili kupata fedha za maandalizi kwa ajili ya kidato cha kwanza.

Mhitimu katika Shule ya Msingi Nyihogo, Kahama mkoani Shinyanga, Salome Richard, anasema anaamini atafaulu mtihani wa kuhitimu darasa la saba na kuendelea na masomo isipokuwa anasaidiana na wazazi wake kufanya biashara ndogo ndogo za kuuza mboga mitaani ili kupata fedha za kununua mahitaji ya shule atakayopangiwa.

Anasema kuna wakati wanapata changamoto ya kuitwa ndani na wanaume kuuza mboga na kuanza kushawishiwa kwa kupewa fedha ambazo zinazidi thamani ya mzigo walio nao na wale wasiojisimamia wanakubali na kuingia kwenye ngono zembe.

Naye Kevin Bundala, mhitimu wa darasa la saba Shule ya Msingi Nyashimbi wilayani Kahama, anasema ugumu wa maisha katika familia yao ndiyo sababu ya kushirikiana na wazazi kufanya biashara hizo. Anasema wakikaa nyumbani wanaweza kujiingiza kwenye vitendo viovu vikiwamo matumizi ya dawa za kulevya na ngono.

Mhitimu mwingine kutoka Magu mkoani Mwanza, Melison Samwel, anasema kwa sasa anajihusisha na uuzaji wa maji na kuwa ananunua toroli lenye madumu tisa kwa Sh.300 na kuuza mitaani kwa Sh.2,000, hivyo kujipatia faida ya Sh.1,700 kwa tripu moja.

"Kwa siku nina uwezo wa kupata tripu zaidi ya tano. Wateja wangu ni watu wa hotelini na kwenye nyumba za watu. Nilianza tu nilipomaliza shule. Fedha ninazopata natunza kwa ajili ya kuwasaidia wazazi kununua baadhi ya vifaa vya shule endapo nitachaguliwa," anasema.

Kuhusu masomo ya awali ya sekondari Samwel anasema bado hajaanza kwa kuwa ni lazima alipe fedha kabla ya kuanza na uwezo wa wazazi wake kifedha si mzuri. Anasema baada ya shughuli zake za kila siku, wakati mwingine anamtumia dada yake ambaye yuko kidato cha tatu kumweleza baadhi ya mambo yaliyoko sekondari.

### MZAZI AFUNGUKA

Baadhi ya wazazi wenye watoto wanaojihusisha na shughuli za utafutaji wakisubiri kuanza kidato cha kwanza, akiwamo Suzana Albogasti, alisema ni wakati wa mtoto wake ambaye kwa sasa anauza dukani kumsaidia katika kutafuta fedha za kidato cha kwanza.

Anasema hali hiyo itamsaidia kutokujiunga na makundi yasiyo salama kitabia.

"Nashukuru amemaliza vyema hivyo siwezi kuruhusu aanze kuzurura ovyo. Dunia ya sasa imeharibika ni bora anisaidie kutafuta hela. Nina imani atafanya vizuri akianza masomo," anasema.

### WADAU WANENA

Diwani wa Bukandwe, Magu mkoani Mwanza, Marco Minzi, anawashauri wazazi na walezi wa wanafunzi waliohitimu elimu ya msingi kutenga muda wa watoto wao kufanya shughuli za nyumbani na muda wa kujisomea kwa ajili ya maandalizi ya hatua nyingine ya elimu ya sekondari.

Anasema wakati huu si sahihi kwa mtoto kupatiwa majukumu ya muda mrefu ikiwa ni pamoja na kulima, kufanya biashara na kuchunga mfugo hali inayomfanya mtoto kusahau wajibu ulioko mbele yake wa kuendelea na masomo ya sekondari. Anasema ni wajibu wa mazazi na mlezi kuhakikisha anatenga muda wa mtoto kufanya shughuli hizo na kupata muda wa kutosha wa kujisomea.

Meneja wa Shule ya Rwepa's iliyoko Mhungula Manispaa ya Kahama, Frank Samweli, alisema kipindi chote cha shule walikuwa wakiwafundisha watoto maadili mema ili watakapokuwa uraiani wasije kujiingiza kwenye vitendo viovu na sasa jukumu la malezi libaki kwa wazazi na walezi, hivyo wana wajibu wa kuwaandaa na masomo ya mbele na sio kuwatwisha majukumu.

Mwanasheria na Kaimu Katibu Mkuu wa Shirika la Kutetea Haki za Binadamu (SHIHABI), Onesmo Daudi, anasema mzazi haruhusiwi kubebesha majukumu mtoto kwa mujibu wa sheria ya mtoto namba 21 ya mwaka 2009 na endapo atabainika atachukuliwa hatua za kisheria.

"Mtoto anapotumikishwa pindi amalizapo darasa la saba au kidato cha nne, anajiona kama ndio mwisho wake wa elimu na matokeo kusahau ndoto zake za kielimu. Tuache kubebesha majukumu watoto yanayopaswa kubebwa na watu wakubwa wasio wanafunzi," anasema Daudi.

Ofisa Elimu Sekondari Manispaa ya Shinyanga, Lucas Mzungu, anawaagiza maofisa elimu kata kuwasaka na kuwapeleka shuleni wanafunzi wote ambao wamehitimu elimu ya msingi ambao wamekuwa wakizurura mitaani, ili wasome masomo ya Kiingereza kwa ajili ya kujiandaa na kidato cha kwanza mwakani.

Anasema hali ya watoto kuendelea kuranda mitaani na hata kuuza vyakula ni hatari kwa maandalizi ya kuingia kidato cha kwanza.

Anasema utaratibu wa serikali ambao ulianzishwa ni kwamba wanafunzi ambao wamehitimu elimu ya msingi, wanapaswa kuanza masomo ya Kiingereza katika shule ambazo ziko jirani badala ya kuzurura mitaani au kujishughulisha na biashara ndogo ndogo.

"Wakasome masomo hayo tena bure kwa shule ambazo wako jirani nazo. Hii itasaidia kumwandaa mtoto vizuri na maandalizi ya kidato cha kwanza," alisema Mzungu.

**Imeandaliwa na Neema Emmanuel (MWANZA), Elizaberth Faustine (MWANZA), Vitus Audax (MWANZA), Marco Maduhu (SHINYANGA), Shaban Njia (KAHAMA)**

## HABARI KITAIFA

# Balozi Hungary akunwa usimamizi wa Tanzania sera fedha, uchumi

**Na Benny Mwaipaja,** DAR ES SALAAM

BALOZI wa Hungary nchini mwenye makazi yake Nairobi, Kenya, Zsolt Mészáros, ameipongeza Tanzania kwa kusimamia vyema sera zake za fedha na uchumi, hatua iliyoifanya iendelee kuimarika kiuchumi.

Kutokana na hali hiyo, ameahidi kwamba nchi yake itaongeza ushirikiano kwa faida ya nchi hizo mbili.

Mészáros aliyasema hayo jana katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha, Dar es Salaam, alipokutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba.

Alisema nchi yake imekuwa ikifuatilia kwa karibu maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Tanzania ikiwamo hatua kubwa inazochukua kuvutia uwekezaji wakiwamo wanaotoka nchini mwake.

Balozi huyo aliahidi kuwa nchi yake iko tayari kushirikiana na Tanzania katika kuchangia maendeleo hususan katika sekta za huduma za jamii kama vile maji kupitia mpango wake maalumu wa kushirikiana na serikali ujulikanao kama 'Tied Aid Facility'.

Waziri Nchemba alisema uchumi wa Tanzania umeimarika na katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha wa 2024/25, umekua kwa wastani wa asilimia 5.6 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia tano katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha uliopita.

Alisema makadirio ya ukuaji wa uchumi katika kipindi cha mwaka 2024/25 ni wastani wa asilimia 5.4 na asilimia 5.8 mtawalia kutokana na miongozo na usimamizi mzuri wa uchumi wa serikali.

"Takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) Agosti, mwaka huu, zinaonesha kuwa uchumi wetu umeimarika licha ya kuwapo kwa changamoto mbalimbali huku ukuaji huo ukichangiwa kwa kiasi kikubwa na sekta za ujenzi, kilimo, fedha na sekta ya bima," alisema Dk. Nchemba.

Aidha, Dk. Nchemba alimweleza balozi huyo kuwa kasi ya mfumuko wa bei imedhibitiwa na kuwa katika kiwango cha asilimia 3.1 na kuwa katika wigo wa tarakimu moja.

Alisema kiwango kilichokubaliwa pia katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) zilizoweka ukomo wa asilimia nane na kiwango cha nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) cha asilimia tatu hadi saba.

Alisema uimara wa uchumi wa Tanzania umethibitishwa pia na mashirika yanayofanya tathimni ya hali ya uchumi wa nchi mbalimbali duniani ikiwamo Taasisi ya Moody's ambayo hivi karibuni, iliipandisha daraja Tanzania kutoka Daraja B2 kwenda Daraja B1 na Taasisi ya Fitch ambayo imeipa Tanzania Daraja la B+ yenye Mtazamo Chanya.

Dk. Nchemba alisema hatua hiyo imeifanya Tanzania na sekta binafsi kuaminiwa zaidi na taasisi za fedha za kimataifa kwamba zinaweza kuyafikia masoko ya fedha ya kimataifa na kuvutia uwekezaji wa mitaji na teknolojia kutoka maeneo mbalimbali duniani.

Alitoa wito kwa wawekezaji kutoka Hungary kuwekeza nchini katika maeneo balimbali watakayoona yanawafaa kutokana na serikali kuweka mazingira bora yanayovutia uwekezaji.






Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (wa pili kulia), akizindua kituo atamizi cha mkonge katika jengo la Bodi ya Mkonge, jijini Tanga jana. Wengine ni Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge, Sady Kambona (kushoto) na wa pili kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Japhari Kubecha. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Polisi yaonya watu kutumia mgongo wake kufanya uhalifu

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi limeonya baadhi ya watu kufanya matukio ya uhalifu yakiwamo ya watu kupotea au kutekwa kwa kutumia mgongo wa chombo hicho.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam katika kongamano la kitaifa dhidi ya matukio ya kupotea na kutekwa, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, alisema mara kadhaa jeshi hilo limekuwa likikamata wahalifu wanaojifanya askari polisi au kutoka mamlaka zingine za dola.

Kongamano hilo limeitishwa na Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) na kushirikisha wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini, wanasiasa na Jeshi la Polisi.

Kamanda Muliro alitoa ufafanuzi huo baada ya kuulizwa swali kuhusu tukio la mauaji ya kiongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Ali Kibao, ambaye alikutwa ameuawa baada ya kuchukuliwa kwenye basi na watu waliojitambulisha askari waliokuwa na silaha.

Akifafanua kuhusu matukio ya aina hiyo, Kamanda Muliro alisema mara kadhaa wamekamata watu wanaojifanya askari wa Jeshi la Polisi au kutoka vyombo vingine vya ulinzi na usalama.

"Kwa hiyo kusema kwamba wale ni polisi kabla ya uchunguzi haujafikia mwisho, ninadhani tusijenge utamaduni huo. Tujenge tabia ya kuheshimu mamlaka za kiuchunguzi ili zifanye kazi katika kuitafuta haki. Tunaweza kujikuta tunaumiza watu ambao hawana makosa halafu baadaye tukapata majuto.

"Likitokea tukio ninashauri wanazuoni na wanataaluma wa masuala ya kisheria tujenge tabia ya kuviamini vyombo vya kiuchunguzi, haiwezekani tukaenda kwa mfumo kwamba kila jambo tume.

"Mnakumbukumbu kuna kipindi serikali fulani kila jambo tume, ilikuwa kama miradi ya watu kula fedha tena ikapigiwa kelele, lazima tuamini vyombo vipo kisheria vifanye kazi," alisema.

Kamanda Muliro alisema endapo litatokea jambo halijakwenda sawa, watumie mifumo ambayo ametumia Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) ya watu kuzungumza. Alisema haiwezekani kila chombo kilichoundwa kisheria wakakikataa.

Kuhusu kuwapo chombo huru nje ya polisi, Kamanda Muliro alisema: "Nilitaka nikukumbushe jambo moja la kuheshimu vyombo vyetu kama tabia ya kuheshimu wanasheria wetu kuheshimu majaji wetu.

"Tusirudi kwenye ukoloni. Wapo waliosoma vizuri lazima tuwaheshimu. Mamlaka hizi zimefanya kazi kubwa sana pamoja na dosari za kiuchunguzi dhidi ya baadhi ya waliopotea au kutekwa. Iko idadi kubwa ya waliotekwa na kupotea wamepatikana. Zaidi ya watu 37 walipotea na wamepatikana kwa sababu tofauti," alisema.

Kamanda Muliro alitaja baadhi ya sababu za matukio ya aina hiyo katika uchunguzi wao ni kulipiza kisasi, masuala ya hasira au madai ya kudhulumiana, ushirikina na hapo wanaotumia mwamvuli wa Jeshi la Polisi kujitambulisha kama askari.

Kadhalika, alikanusha kuwa si kila aliyepotea au kutekwa ni CHADEMA kama mitazamo ilivyo na kufafanua kwamba baadhi ya watu aliofuatilia katika uchunguzi katika visa kama 37 hawakuwa wa chama hicho bali kutoka vyama mbalimbali.

"Lakini kwenye uchunguzi ukihoji ukienda mbali unakuta si CHADEMA, CCM au ACT -Wazalendo unaweza kukuta ni wa vyama tofauti, lakini amekutwa na kadhia hii. Ndiyo maana ninazo baadhi ya sababu zaidi ya nane ambazo zinasababisha kutokea kwa aina hii ya matukio wakati tunachunguza mambo hayo.

"Baadhi ya masuala ya kiuchunguzi yanatakiwa kabla ya hayajafanyiwa uchunguzi tusiyahukumu kwa sababu unaweza kukuta sababu za matukio yale ni tofauti na namna unavyoelezea," alisisitiza.

Alipoulizwa kama ameshindwa kukabiliana na matukio hayo mkoani humo, alisema somo la kiuchunguzi liko tofauti hasa wanapofuata misingi ya haki bila kuonea mtu au kubambikiza kesi.

"Ukifanya upelelezi kwa presha unaweza kujikuta unabambikiza kesi mtu au watu kwa ajili ya kuridhisha watu uchunguzi si kama hesabu za kidato cha pili," alisema.

**MWABUKUSI ALONGA**

Rais wa TLS, Boniface Mwabukusi, alisema wako hapo kwa sababu jamii yoyote iliyostaarabika na inayoamini misingi ya utu na uadilifu kama inavyoainishwa chini ibara ya 9 ya Katiba. Alisema kunapotokea changamoto hutafuta njia bora na sahihi na kutatua.

"TLS inaamini kunapokuwa na tatizo jambo la kwanza na la msingi ni kukubali kuwapo wa tatizo husika. Ukishatambua na kukubali tatizo unaligeuza kuwa changamoto na kulitafutia majawabu na siyo majibu. Uwapo wa TLS ndio kiungo kizuri kati ya wananchi na seriali yao, kwa mujibu wa sheria kifungu cha 4," alisema.

Mwabugusi alisema ni lazima wawe na sehemu ya kukutana na kuzungumza kwa sababu ndio mahali kunakotoa fursa ya kuelewa kile mwenzake amefanya na kupitia hapo wanakubaliana waendaje.

"Unapomwona mwenzako amekwenda tofauti unasema wewe si mwenzetu. Kukutana kwa pamoja ni fursa zetu kuzungumza yanayotusibu kwa njia ya staha na katika uhalisia wake na kwa namna ya kutafuta ufumbuzi wa changamoto hii, huku taifa likibaki imara na salama kwa sababu tuna taifa moja tu," alisema.

Alisema TLS kupitia wajibu wake kifungu cha 4, wameona wakutane na wadau hao, badala ya wengine kutoa kauli na wengine kukanusha.

"Biblia inasema si mtu mzima atafutaye mganga, bali mgonjwa atamanie kupona. Kama ninakulaumu halafu nikaseme, ninataka kukaa mwenyewe bila wewe kunisikiliza na mimi kusikiliza tutafikia wapi mwafaka?" alihoji.

Baadhi waliochangia katika mkutano huo ni pamoja na Askofu Mkuu wa Kanisa la Morabvian la Uamsho Tanzania, Emmaus Mwamakula, ambaye, alitoa wito wa kukaa kama baraza la watu wazima kuongea masuala hayo.

"Rais ana uwezo mkubwa kuita viongozi hasa wa dini na wastaafu wakubwa ndani ya nchi hii kujadiliana namna ya kutoka katika uchafu huo," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa Shura ya Maimam, Shekhe Issa Ponda, alisema mjadala wao ujikite namna ya kuzuia utekaji na mapendekezo yaliyotolewa ni namna gani ya kutunga sheria.

"Hawa watekaji ni watu waliokamilika wana vikisi, wana magari na suala. Kwa lugha nyepesi kuna vikosi vya kuteka watu, lazima tujue asili yake na tunavizuiaje," alisema.

RIPOTI MAALUM-2

# Kibong'oto yaanika ukubwa tatizo kifua kikuu migodini

Na Romana Mallya

**SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana, iliangazia mgonjwa wa TB sugu alivyonusurika kifo mara mbili na baada ya kupona kisha kuitunuku tuzo maalum Hospitali ya Rufani ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto (KIDH), iliyomtibu. Sehemu ya pili ya ripoti hii inabainisha ukubwa wa tatizo hili migodini. Endelea...**

---



Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto (KIDH), Dk. Leonard Subi.

SAMWELI Rugemalila, ni mmoja wa wachimbaji wadogo Mirerani mwenye wafanyakazi 60 ambako baadhi ya wagonjwa wa TB sugu wanatajwa kutokea katika mgodi huo maarufu kwa uchimbaji wa Tanzanite.

Rugemalila anakiri katika eneo lake la mgodi kwa vipindi tofauti ikiwamo mwaka huu, wafanyakazi wake baada ya kupimwa walikutwa na maambukizi ya ugonjwa huo.

"Kwa mwaka huu (2014) wafanyakazi wangu baada ya kupimwa afya zao katika mgodi wangu, ni mmoja tu ambaye alikutwa na TB na kuanza matibabu mara moja ili kutoruhusu maambukizi zaidi kwa wenzake."

Hata hivyo, akilinganisha miaka zaidi ya miwili iliyopita, Rugemalila anasema kwa sasa hali ya ugonjwa huo katika mgodi imeimarika.

Anasema wagonjwa si wengi kwa sababu mara kwa mara mashirika yanayojishughulisha na masuala ya tiba, huwafikia kutoa elimu na kupima wafanyakazi.

"Kesi nyingine ya wafanyakazi katika mgodi wangu kukutwa na TB ilikuwa ni zaidi ya miaka miwili na waligundulika wafanyakazi wawili tu. Mwaka huu mwezi wa pili walikuja wataalamu wa afya kutoka katika mashirika yanayojishughulisha na ugonjwa huu.

"Wafanyakazi walipewa elimu na baadaye kupimwa afya na ni mmoja tu mwenye jinsia ya kiume, mwenye umri wa miaka 55 alikutwa na TB na huyu alikuwa ametoka mgodi mwingine kuja hapa kwangu. Alianza matibabu yake na sasa yupo kazini," anasema.

Rugemalila anasema huduma za matibabu zimesogezwa karibu. Mbali na Hospitali ya Kibong'oto, sasa Mirerani kuna zahanati ambayo wagonjwa wa TB wanapobainika migodini, kupatiwa dawa hapo.

"Mfanyakazi aliyeugua wewe kumwomba na kuongea naye ataona kama nimemwanika aliugua TB. Ninachoweza kukueleza TB migodini ipo, lakini kulinganisha na huko nyuma, hali kwa sasa ni nzuri kwa sababu matibabu yake yamesogezwa na elimu zinatolewa mara kwa mara.

"Kwa mwaka huu hadi mwezi Agosti katika mgodi wangu, mashirika yanayotoa elimu na kupima yameshakuja mara tatu, hii inasaidia sana.

"Wito wangu kama mmiliki wa mgodi kwa kushirikiana na serikali, tuendelee kuhamasisha vijana upimaji TB wa mara kwa mara kwa sababu dawa zipo na matibabu ni bure. Tusiposhirikiana kwa pamoja jambo hili halitakwisha na TB ni ugonjwa wa kuambukiza," anasema.

Julai, 2023, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Makatibu Wakuu na Mameneja Mpango wa Programu za TB kutoka nchi 15 barani Afrika unaofanyika kwa jijini Arusha. Mkutano huu pamoja na mambo mengine ulijadili namna nchi za Afrika zinaweza kuja na ubunifu pamoja na mikakati mipya ya kutokomeza TB Afrika na duniani kwa ujumla ifikapo mwaka 2030.

Wakati kukiwa na mikakati hiyo, Hospitali ya Rufani ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto (KIDH), iliyoko Wilaya ya Siha, Kilimanjaro, kupitia Mkurugenzi wake, Dk. Leonard Subi, katika mahojiano maalum na Nipashe, anaweka wazi hali ilivyo hospitalini hapo.

"Kuhusu hali hospitalini hapa kwa wagonjwa wa TB sugu, wako wengi ambapo kwa mwaka hufikia wagonjwa hadi 400.

"Tukiangalia kiidadi inapungua. Waathirika ni makundi yote kuanzia umri wa miaka 20 hadi 59 lakini wanaume ni zaidi kutokana na shughuli zao na wengi wapo katika migodi," anasema.

Katika mahojiano hayo yaliyofanyika Agosti 6, mwaka huu, Mkurugenzi huyo anafafanua kuwa wanaposema magonjwa ambukizi wanamaanisha magonjwa yote yenye umuhimu wa pekee katika jamii ya kuambukiza yanayosababishwa na virusi, bakteria, fangasi na protozoa.

"Sisi ndio wenye jukumu hilo tangu mwaka 2010 Hospitali ya Kibong'oto ilipotangazwa katika gazeti la serikali namba 828 la Novemba. Suala la TB kwetu ni moja ya ugonjwa kipaumbele ndio alama ya hospitali maana ndiko ilikoanzia. Lengo la sasa ndio hospitali pekee ya rufani ya ugonjwa wa TB sugu nchini.

"Bahati nzuri serikali inawagharamia wagonjwa wote wa TB ya kawaida na sugu katika matibabu na vipimo," anasema.

Anasema wale wa TB sugu huwa wanawafuata nyumbani kokote waliko nchini endapo Mganga Mkuu wa Mkoa husika atasema huyo ni mgonjwa wa rufani.

"Si lazima kuja hapa Kibong'oto na hii ni kwa sababu tumeshatoa mafunzo na tumeshajenga uwezo na tunawapelekea dawa waliko kwa gharama za serikali.

"Tunawalipia vipimo vyao vya maendeleo vya kimatibabu huko waliko. Hospitali yetu inatoa huduma hizo za kibingwa.

"Na wengine tunakuta wana usugu wa dawa, yaani za mstari wa kwanza wamezimaliza, za mstari wa pili wamemaliza, tunapambana nao mpaka kuhakikisha wanapona," anasema.

Dk. Subi anasisitiza kwamba serikali inawapatia huduma nzuri za kimatibabu, dawa pamoja na lishe ambapo hupatiwa chakula mara nne kwa siku.

"Wanapatiwa chakula bora ambacho hata nyumbani kwao yawezekana hawana. TB sugu inatibiwa kwa matibabu ya miezi tisa kwa hapa Tanzania. Japo tunataka kubadilisha kuwa miezi sita baadaye.

"Hapa hospitalini wagonjwa wa aina hii tunakaa nao takriban miezi sita. Wanalazwa pale wanapata huduma zote za kibingwa na ubingwa bobezi, lakini pia wagonjwa hao hao tunawapa tiba ya saikolojia.

"Kwa nini tiba ya kisaikolojia. Mtu anatoka nyumbani kwake anaishi nje zaidi ya miezi sita hivyo anahitaji tiba ya saikolojia ili wasikate tamaa. Katika tiba hii wengine huwa tunawapeleka mbuga za wanyama kule wanakwenda wanafurahi na kufurahisha akili na kuwaondolea msongo wa mawazo," anasema.

Dk. Subi anaelezea tuzo maalum ambayo hospitali imeipokea kutoka kwa Labowa Ingwagwi, mkazi wa Babati mkoani Manyara, mmoja wa mgonjwa aliyewahi kutibiwa hospitalini hapo kuwa imeongeza motisha kwa watumishi wakiwamo waliokuwa wanamhudumia.

Anasema mwanamume huyo alifikishwa hospitalini hapo baada ya kupewa rufani na alipatiwa matibabu yaliyochukua muda mrefu hadi kupata nafuu.

Ofisa Muuguzi Hospitali ya Kibong'oto, Sarah Matoi, aliyehudumu hospitalini hapo tangu mwaka 1994 na kuwa miongoni waliomtibia Ingwagwi, anasema tuzo maalum waliyopokea kutoka kwa mgonjwa huyo wakati huo ni ya kipekee kwao na imewaongezea ari ya kufanya kazi kwa wito zaidi.

Anasema wagonjwa wengi hutoka maeneo ya mbali na wanapokaa muda mrefu hospitalini baadhi hadi miezi 18, hukumbuka nyumbani.

"Fikiria mtu unachomwa sindano miezi miwili mfululizo (siku 60), mgonjwa anavurugika akili, anapata msongo wa mawazo. Tunamshukuru Mungu wagonjwa wanapona vizuri na tunawapa ushauri ili tatizo lisijirudie," anasema.

Matoi anasema wamekuwa makini kuhakikisha wahudumu wa afya hawapati maambukizi kwa kutumia vifaa vya kujifunika.

Pia, kuangalia mazingira upepo unakoelekea na kuhakikisha hewa inaingia na kutoka wodini na mara kwa mara kutoa elimu kwa wagonjwa wanapokohoa wazibe mdomo.

"Mgonjwa akitumia dawa ndani ya wiki mbili vimelea vinakuwa havina uwezo wa kuambukiza kwa haraka. Asilimia kubwa wagonjwa wetu wanatoka migodini hususan Mirerani.

"Kwa miaka ya nyuma 1998-2000 wagonjwa wa nje tuliokuwa tukipokea kwa siku walikuwa ni kuanzia 100, 2002-2024 kwa siku kliniki ya nje huwa karibu 60," anasema Matoi.

**Itaendelea kesho**

# CHADEMA yatuma salamu uchaguzi Zanzibar

**Na Suleiman Rashid Omar,** PEMBA

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Zanzibar, Salim Mwalimu Juma, ametuma salamu kwa wanasiasa kuwa mshindi wa uchaguzi mkuu ujao wa Zanzibar atatoka chama chake kutokana na anavyoendelea kujipanga.

Alisema kuporomoka kwa kutopendwa kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM), CHADEMA ina uhakika wa kushinda urais Zanzibar kutokana na ilivyojipanga kuongeza idadi ya wanachama na pamoja na kuungwa mkono na CCM na ACT -Wazalendo hasa kisiwani Pemba.

Akizungumza na wajumbe wa mabaraza ya uongozi wa CHADEMA Kanda ya Pemba kwenye ukumbi wa Kibirinzi mjini Chakechake, alisema katika uchaguzi mkuu ujao, chama chake kimedhamiria kuingia kikiwa na uhakika wa kushinda kwa kuwa wameshasoma uchaguzi uliopita.

"Katika chaguzi zilizopita tulikuwa hatuingii tunakaa mlangoni tu tunachungulia ila mara hii tutaingia wote kifua mbele na kwa kujiamini," alisema.

Alisema miaka yote CHADEMA ilikuwa ikikaa mlangoni na kuchungulia kujua harakati na mbinu zinazotumiwa na CCM na ACT Wazalendo na sasa iko imara kukabiliana na uchaguzi ujao.

Salum aliwasihi wana CHADEMA kushikamana kujenga umoja na kuachana na utegemeo wa aina yoyote wakati huu ambao wananchi wameleta matumaini ya kujiunga kwa wingi katika chama hicho.

Alisema tayari katika uchaguzi unaoendelea ndani ya chama, wamekwisha kufanya uchaguzi kwenye matawi yote ya Pemba na jambo linalotia matumaini ni kuwa hivi sasa kuna baadhi ya matawi yana zaidi ya wanachama 80 wakati ili kuunda tawi wanahitajika wanachama 50 tu.

Naye Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Zanzibar, Said Issa Mohamed, alisema wanachama wengi wa vyama vya siasa, hujenga makundi wakati wa uchaguzi wa ndani ya vyama vyao na uongozi unaposhindwa kurekebisha huwa sababu ya chama kusambaratika na kukosa ushindani wakati wa uchaguzi mkuu. Alisema majungu, fitna na mgawanyiko utakaojitokeza kwa njia yoyote haukubaliki na unafaa kupigwa vita usije kukigawa chama wakati huu ambao kimekwisha kukubaliwa na wananchi wengi wanajiunga.

Said alisema inavyoonesha sasa, CCM, ACT-Wazalendo na Chama cha Wananchi (CUF) vinakosa wafuasi na kupungua umaarufu lakini CHADEMA inazidi kupata umaarufu kwa kasi, hivyo hawana budi kujizatiti na kuzidi kujipanga ili kufanikisha malengo yao ya kuchukua dola.

Aliwataka wana CHADEMA kuona fursa zilizoko kwa kuwa chama kikishachukua dola, kina nafasi nyingi za uteuzi kiasi kuwa watalazimika kuchukua watu nje ya chama kama watu hawatazingatia na kujiunga kwa wingi ili kukimbilia fursa hizo ambazo zinakuja.

Pia aliwataka wana Chadema kufanya kazi kwa kuwa hakuna sababu ya kushindwa katika uchaguzi wowote unaokuja.

# Majaliwa ahimiza matumizi mifumo ya kielektroniki ukusanyaji mapato

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka maofisa masuhuli katika halmashauri zote nchini waweke msisitizo wa kutumia mifumo ya kielektroniki katika makusanyo badala ya kukusanya kwa fedha taslimu.

Amesema kwa kufanya hivyo kutasaidia kuongeza mapato katika maeneo yao na kuepuka vishawishi vya kutumia vibaya fedha za umma ambazo zinakusanywa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Majaliwa aliyasema hayo jana wakati akizungumza katika kikao na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Temeke, Dar es Salaam.

"Suala la mapato ni lazima mliwekee msisitizo ili tupate matokeo mazuri katika halmashauri zetu," alisema.

Majaliwa alitoa wito kwa wakurugenzi wa halmashauri kutumia mapato ya ndani katika kutekeleza miradi ya maendeleo badala ya kusubiri fedha kutoka serikali kuu pekee.

Aliwataka watumishi wa umma kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na uaminifu ili mipango na malengo ya serikali ya kuwahudumia Watanzania yaweze kutimia. Alisema watumishi wa umma ni wahudumu wa wananchi, hivyo wanapaswa kuwahudumia ipasavyo katika maeneo yao na kutatua kero zao.

"Sisi tunataka tuone mkifanya kazi kwa bidii, uadilifu, uaminifu usipofanya hivyo utakuwa unakosa sifa za kuwa mtumishi wa umma," alisema.

Majaliwa aliwataka watumishi wa umma kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika maeneo yao kwa kuangalia hatua iliyofikiwa na sehemu iliyobaki, ili mpaka kufikia Juni mwakani miradi hiyo iwe imefikia zaidi ya asilimia 95 ya utekelezaji.

Kadhalika, aliwataka kusimamia maendeleo ya kiuchumi kwa wananchi na kutengeneza mazingira wezeshi ya kujiendeleza kiuchumi.

"Punguzeni urasimu ili tujenge imani kwa tunao wahudumia, makundi yote yaliyo katika maeneo yenu yakiwamo ya vijana, wazee, wanawake na wenye ulemavu, lazima tuwafikie na kusimamia uchumi wao," alisema. Majaliwa ameweka jiwe la msingi la uzinduzi wa bweni na bwalo katika Shule ya Sekondari ya Kibasila iliyoko wilayani humo, uliogharimu Sh. bilioni 1.13.



Mbunge wa Jimbo la Kiteto, mkoani Manyara, Edward Ole Lekaita, akizungumza kwenye mkutano wa hadhara wa kuelezea mafanikio na kusikiliza changamoto na kero za wananchi katika Kata ya Engusero, mwishoni mwa wiki. **PICHA: GIFT THADEY**

# Vitongoji 166 Morogoro kuondolewa shida umeme

**Na Frank Monyo**

WAKAZI katika vitongoji 166 mkoani Morogoro wanatarajiwa kuondokana na shida ya umeme baada ya serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kumtambulisha mkandarasi aliyeshinda zabuni ya kupeleka umeme ili kuanza kazi.

Mradi huo wenye gharama ya Sh. bilioni 17.9 unatarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha miezi 24 na utakapokamilika utanufaisha zaidi ya kaya 5,478.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya kumtambulisha mkandarasi huyo ambaye ni kampuni ya SINOTEC, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha hizo pamoja na kuipongeza REA kwa kusimamia vyema maono ya Rais kuhakikisha wananchi wa vijijini wanapata maendeleo kupitia upatikanaji wa nishati ya umeme.

"Morogoro ni mkoa wa kimkakati, mkoa wa uzalishaji na tumejipanga kuwa namba moja katika kilimo nchini. Kuwapo kwa umeme maeneo ya vijijini kutasaidia kuongeza thamani ya mazao ya kilimo.

"Umeme ndio nguzo namba moja katika kuongeza thamani mazao ya kilimo. Tuendelee kumpongeza na kumshukuru Rais Samia kwa kutoa fedha zinazokwenda kuwezesha zaidi ya vitongoji 166 kupata umeme," alisema Malima.

Aliwataka wananchi kutunza miundombinu ya umeme na mkandarasi kuhakikisha anatekeleza mradi huo ndani ya muda uliopangwa na kwa viwango vya ubora vinavyokubalika.

Akitoa taarifa ya upelekaji wa umeme vijijini, Msimamizi wa Miradi ya REA Kanda ya Kati, Mhandisi Aneth Malingumu, alisema kuwa kati ya vijiji 669 mkoani humo, vijiji 652 sawa na asilimia 97.5 vimefikiwa na nishati ya umeme.

Malingumu alisema vijiji 17 vilivyobaki viko katika hatua za mwisho za ukamilishaji na kabla ya Oktoba 20 mwaka huu, vitakuwa vimepata umeme.

Mhandisi Malingumu alisema Morogoro unajumla ya vitongoji 3,369 na kati ya hivyo, vitongoji 1,655 sawa na asilimia 49 tayari vimepatiwa umeme.

"Katika kipindi cha miaka miwili tunategemea vitongoji 455 vya mkoa huu kupatiwa umeme. Ndani ya hivyo, 289 mkandarasi tayari yuko kazini na anaendelea na kazi kupitia mradi wa ujazilizi yaani Densification IIB.

"Vitongoji 166 vitapatiwa umeme kupitia mradi huu ambao tunatambulisha mkandarasi wake leo kwa gharama ya Sh. bilioni 17.9," alisema Mhandisi Malingumu.

Alimwakilishia Mkuu wa Mkoa huyo kwamba REA imejipanga vyema kuhakikisha umeme unafika vijiji vyote na safari ya kupeleka umeme katika vitongoji inaendelea kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mwakilishi wa Kampuni SINOTEC, Zhang Jianguang, aliahidi kutekeleza mradi huo kwa wakati na kwa ubora na tayari maandalizi muhimu ameanza.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni muhimu kudhibiti mianya ya ukwepaji, kuongeza walipakodi

**RAIS** Samia Suluhu Hassan juzi alizindua Tume ya Rais ya Kutathmini na Kushauri kuhusu Masuala ya Kodi na kubainisha kuwa mrejesho alioupata katika ukusanyaji wa kodi unaonesha kuwapo kwa malalamiko ya mianya ya ukwepaji wa kodi, makusanyo kidogo, huku mengi yakiingia mifukoni mwa watu.

Hatua hiyo, kwa mujibu wa Rais Samia inasababishwa ma baadhi ya watumishi wa serikali kutokuwa waadilifu na kuwapo kwa utaratibu usioridhisha katika utoaji wa misamaha ya kodi kwa wawekezaji.

Rais alisema pamoja na kuwapo kwa mianya hiyo ya ukwepaji kodi, idadi ya walipakodi ni ndogo kulinganisha na zaidi ya Watanzania milioni 60 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi. Alisema idadi ya walipakodi ni zaidi ya milioni mbili kati ya watu milioni 66 na kwamba wakitoa watoto na watu wengine ambao hawastahili kulipa kodi, hawapungui milioni 37 ambao wanaweza kulipa kodi.

Pamoja na walipakodi kuwa wachache, Rais alisema serikali imeimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato na kuijengea uwezo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kuimarisha mazingira ya kufanya biashara, hivyo kuchangia kuleta matokeo chanya kwa makusanyo ya kikodi ambayo yameongezeka kutoka wastani wa Sh. bilioni 850 kwa mwezi mwaka 2015 hadi wastani wa Sh. bilioni mbili kwa mwaka 2023, katika ripoti iliyotolewa hivi karibuni na TRA, kuna mafanikio makubwa baada ya kukusanya mwezi uliopita zaidi ya Sh. trilioni tatu.

Mwasisi wa taifa la Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, aliwahi kusema nchi yoyote isiyokusanya kodi lazima itakuwa na matatizo yakiwamo ya rushwa. Hivyo ndivyo inavyosadifu kutokana na kauli ya Rais kuhusu kuwapo kwa mianya ya ukwepaji kodi na baadhi ya watumishi wasio waaminifu kuchepusha fedha za umma na kuziingiza katika mifuko yao.

Kutokana na uwapo wa hali hiyo, kuna uwezekano mkubwa hata takwimu zilizotolewa na TRA kuwa makusanyo yamepanda hadi Sh. trilioni tatu zikawa ndogo. Ni dhahiri kwamba kama mianya ya ukwepaji kodi ikazibwa na kuwekwa kwa mazingira rafiki katika ulipaji kodi, kiasi hicho kingepanda hata kufikia zaidi ya Sh. trilioni nne. Kwa mantiki hiyo, kazi kubwa inapaswa kufanyika kwa kuziba mianya hiyo ikiwamo kuchukua hatua dhidi ya baadhi ya watumishi wanaosababisha serikali kukosa mapato kwa sababu mbalimbali.

Katika miaka ya karibuni, kwa mfano, ilishuhudiwa serikali ikitumia vyombo vya dola kama vile polisi wakiwa na bunduki wakienda kudai kodi kwenye sehemu za biashara. Hali hiyo ilisababisha taharuki na kuwafanya baadhi ya wafanyabiashara kufunga shughuli zao na kukimbilia nchi zingine.


Sambamba na kutumia mitutu ya bunduki kudai kodi, baadhi ya maofisa wa TRA kwa kushirikiana na askari polisi walikuwa wakitumia mwanya huo kuwatisha wafanyabiashara na kuwataka wawapatie chochote kitu na waliokuwa wakigoma walikuwa wakitishiwa kufikishwa mahakamani kwa madai ya kukwepa kodi.

Aidha, migomo mbalimbali ya wafanyabiashara katika maeneo kama Dar es Salaam, Arusha, Mwanza ukiwamo ule wa karibuni uliotikisa na kusababisha serikali kukosa mapato, chanzo kikubwa kilikuwa malalamiko ya kubambikiwa kodi. Jambo hilo lilijitokeza pia wakati wa ziara ya Rais mkoani Ruvuma kwamba hata mamalishe na babalishe wamekuwa wanadai TRA wamekuwa wakighasi kwenye shughuli zao.

Kama wahenga wasemavyo yaliyopita si ndwele tugange yajayo, ukurasa mpya unapaswa kufunguliwa ambao utaweka mazingira rafiki kati ya TRA na wafanyabiashara ili makusanyo zaidi yaongezeke. Kuongezeka kwa mapato ya serikali yatokanayo na kodi yataifanya serikali kupunguza mzigo wa kukopa kwa ajili ya matumizi yake na miradi ya maendeleo.

Licha ya kuweka mazingira rafiki, uandaliwe utaratibu kwa TRA kuongeza idadi ya walipakodi kwa kuwasajili ikiwamo wananchi kuweza eshwa kiuchumi kwa kufungua miradi na biashara ambazo zitachangia kuongeza mapato.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Chondechonde madereva wa bodaboda changamkieni fursa kwa manufaa yenu

Na Sabato Kasika

**ZAIDI** ya madereva 200,000 wa bodaboda mkoani Dar es Salaam, wanatarajia kupata elimu ya namna ya kutoa huduma ya kwanza kwa majeruhi na ya usalama barabarani.

Hiyo ni kwa ajili ya usalama wao na watu wengine ambao kwa namba moja au nyingine wawapo barabarani wanaweza kupata ajali.

Elimu hiyo itatolewa na Chama cha Msalaba Mwekundu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo kampuni ya Bia Tanzania (TBL) na Jeshi la Polisi kuanzia mwezi huu hadi Desemba. Mkurugenzi wa Maendeleo ya Matawi ya Chama hicho, Reginald Muhango, alisema wakati wa uzinduzi wa mpango wa kutoa elimu na mafunzo kwa madereva hao.

Katika mpango huo wa kutoa elimu, watajikita pia katika mafunzo ya udereva na sheria ya usalama barabarani ili kusaidia madereva kuwa makini wawapo barabarani.

Kwa malengo hayo, ninaamini kwamba hiyo fursa nzuri kwa madereva hao ili waweze kuichangamkia, kwani itawapa ujuzi zaidi wa kufanya kazi yao kwa ufanisi.

Matamanio ya wadau ni kuona ajali za barabarani zinapungua au kuisha, lakini pia madereva wawe na ujuzi wa kutoa huduma ya kwanza pale inapotokea ajali badala ya kuwa watazamaji tu bila kutoa msaada kwa majeruhi.

Hatua za wadau hao kwenda kutoa elimu kwa madereva hao ili pale wanapopata ajali au wanapokuta ajali, wajue namna kujisaidia au kusaidia wengine ni jambo jema.

Yawe ni matamanio ya madereva kupunguza ajali za barabarani kupitia elimu ambayo itatolewa, kwani hata wenyewe wanakiri kuwa wana ukosefu wa elimu ya udereva.

**Yawe ni matamanio ya madereva kupunguza ajali za barabarani kupitia elimu ambayo itatolewa, kwani hata wenyewe wanakiri kuwa wana ukosefu wa elimu ya udereva.**

Kujifunza udereva uchochoroni usiku, kisha asubuhi mtu anaingia barabarani kubeba abiria, si rahisi kujua sheria za usalama wala kujua jinsi ya kumhudumia aliyepata ajali.

Pamoja na mafunzo hayo, madereva watafaidika na suala la nidhamu kwani wengi wao wamekuwa wagumu kuelewa umuhimu wa nidhamu wapo barabarani.

Ninaeleza hivyo kwa sababu licha ya jeshi kujitahidi kuwaelimisha, baadhi yao hawazingatii, kile ambacho wanatakiwa kukifanya wanapoendesha vyombo hivyo vya moto.

Mazingira ya aina hiyo ni sawa na kuhatarisha maisha yao na ya abiria wao. Hivyo, kama nilivyoelezea, mafunzo hayo ni fursa nzuri kwao kujiandaa kupokea elimu itakayowafanya wawe na ujuzi na pia kuwa makini wakati wote wawapo kazini.

Lakini pia, Shirikisho la Madereva wa Bodaboda na Bajaj mkoa wa Dar es Salaam, linakiri kufanya makosa kutokana na ukosefu wa elimu ya udereva, unaotokana na kile ambacho shirikisho hilo linadai kuwa ni ada kubwa ya kusomea udereva inayotozwa na vyuo vya serikali.

Pamoja na hayo, ninadhani madereva hawana budi kujiongeza kwa kuepuka mazingira yanayoweza kusababisha wakapata ajali, yakiwamo ya kutoheshimu sheria za usalama barabarani.

Imekuwa ni kawaida kuwakuta baadhi ya madereva hao wakivuka taa za kuongezea magari kusimama hata kama haziwaruhusu kuvuka, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wao na abiria.

Itoshe kusema kuwa ni wakati mzuri kwa madereva wote mkoani Dar es Salaam kuchangamkia mafunzo hayo ili hatimaye wawe msaada kwao wenyewe na kwa hata kwa watumiaji wengine wa barabara.

FIKRA MBADALA

# Serikali itie mkono kuondoa kodi ufanisi wa nishati safi ya kupikia



Pascal Mayalla

KWA wengi wa waliozaliwa mijini, hawaijui adha ya kupika kwa kuni. Lakini mamilioni ya kinamama, wanawake, mabibi zetu, mashangazi zetu, wake zetu, watoto wetu, wapenzi wetu, au kwa kifupi wanawake wa Tanzania, wanaoteseka kwa kupikia kuni.

Kutokana na kupikia kuni kwa muda mrefu, kinamama hawa wanaathirika kutokana na matumizi ya nishati ya kuni na mkaa inayoitwa 'tungomotaka' kwa macho yao kuwa mekundu kama yamevia damu. Kule Mwanza, mwaka 1976 mabibi hao walituhumiwa kuwa huo wekundu wa macho yao ni wachawi, hivyo wengi waliuawa kikatili.

Serikali ya awamu ya kwanza chini ya Mwalimu Julius Nyerere, iliingilia kati kukomesha mauaji hayo, hivyo washukiwa wa mauaji ya vikongwe walikamatwa na kuhojiwa kwa mbinu za mateso sana. Matokeo yake, watuhumiwa wawili wa mauaji hayo wa Mwanza, Masaga Makhula Mazenganuka na Isaack Ngw'ana Mkoboko, walipoteza maisha, hivyo Mwalimu Nyerere akakasirika sana kwa nini watu wafe mikononi mwa polisi? Siku hizi hakuna anayejali!

Nyerere alisafisha kuanzia kwa msaidizi wake mkuu Rashidi Kawawa, Mawaziri akiwamo Ali Hassan Mwinyi (Rais wa awamu ya pili) walijiuzulu. Wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama walistaafishwa. Watendaji wa mkoa wa Mwanza, Kamanda wa Polisi wa Mkoa (RPC), Ofisa Usalama wa Mkoa (RSO), Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD) na Ofisa Usalama wa Wilaya (DSO), wote wakapandishwa kizimbani. Kesi ya mauaji Mwanza ilipoanza kunguruma, ndipo nikajua kumbe baba alikuwa nani!

Huo ndio ulikuwa uwajibikaji enzi za Nyerere. Siku hizi watu wanakufa mikononi mwa polisi na si tu hakuna hatua zinazochukuliwa, bali hakuna hata uchunguzi! Kuna mtu amewahi kusikia maendeleo yoyote ya uchunguzi shambulio la Tundu Lissu? Lissu yupo hata kuitwa polisi kuandika tu maelezo, hajawahi kuitwa! Kigugumizi hiki kinawaambia wenye akili, wahusika ni kina nani sasa uchunguze nini ili iweje?

Hali ya nishati nchini Tanzania si nzuri. Watu 22,000 wanapoteza maisha kila mwaka kutokana na magojwa ya upumuaji yanayosababishwa na moshi wa kupikia kwa kuni na mkaa. Kutokana na hali hiyo, kipaumbele cha kwanza kwenye sekta ya nishati ni kuhakikisha gesi inapatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu na inafika kwenye kila nyumba, hivyo kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.

Kitendo cha Rais Samia Suluhu Hassan kulivalia njunga jambo hili la nishati safi ya kupikia ni ukombozi mkubwa sana kwa wanawake wa Tanzania japo kupika kibiashara si kazi ya wanawake ni kazi ya wote na haswa wanaume, hivyo ukombozi huu pia unawahusu.

Kampuni ya Mafuta ya TotalEnergies Marketing Tanzania Limited, imeamua kuunga mkono kampeni ya nishati safi ya kupikia kwa kuanza kusambaza gesi ya kupikia katika vituo vyake vyote zaidi ya 100 nchini ili kufanikisha ndoto ya Rais Samia kufikia mwaka 2030, Watanzania wote wawe wanatumia nishati safi ya kupikia.

Uamuzi huo ulitangazwa na Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Mamadou Ngom, wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Huduma kwa Wateja iliyoanza wiki hii kwa uzinduzi wa kituo cha mafuta cha TotalEnergies Magomeni Makanya, njia ya Tandale Uzuri.

Ngom alisema kutokana na kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Rais Samia, kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, kwa vile TotalEnergies, ndiyo kampuni inayoongoza Tanzania kwa idadi ya vituo vya mafuta, imeamua kumuunga mkono Rais Samia kwenye suala hilo, hivyo itasambaza gesi ya majumbani katika kampeni iitwayo "Jiko Bomba, Pishi Pambe".

Hatua hii ya TotalEnergies si tuu inapaswa kupongezwa, bali kuungwa mkono na wadau wengine wote wenye mapenzi mema na taifa letu, mdau mkuu nambari moja akiwa serikali yenyewe.

Japo Kenya wana bandari ya Mombasa na wanaweza kuagiza gesi ya kutosha, ukisimama mpaka wa Namanga, ukashuhudia idadi ya malori ya gesi kutoka Tanzania kupeleka Kenya, utashangaa na kujiuliza kama wenzetu wana uhaba. Jibu ni hapana bali Wakenya wengi wanatumia gesi hivyo mahitaji ni makubwa wakati Watanzania wengi wanatumia zaidi kuni na mkaa.

Mfanyabiashara wa Tanzania, mwenye Taifa Gas, akaiona fursa ya gesi Kenya, sasa amejenga kiwanda Kenya na kuwahudumia jirani zetu huku Watanzania tukiendelea kuhangaika na kuni na mkaa. Fursa zina utaratibu wa kuzichangamkia, usipochangamkia wewe, wenzako wanazichukua. Sasa Wakenya wengi zaidi wanatumia gesi yetu wakati sisi wenye gesi, tunapikia kuni na mkaa.

Sababu ni moja tuu, majiko ya gesi ni gharama na gesi ni ghali kuliko mkaa wakati kuni ni bure. Ughali huu unachangiwa na kodi na tozo mbalimbali, hivyo kama serikali yetu inachukulia kwa uzito jambo hili basi kupunguzwa kwa kodi na kuwekwa ruzuku katika gesi ya kupikia hakuna mjadala.

**Paskali.**
**+255 754 270403**
**Itaendelea Jumapili ijayo**

# Mbaroni kwa tuhuma wizi wa nguo madukani

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma linawashikilia wanawake watatu kwa tuhuma za wizi wa mali mbalimbali zikiwamo doti 414 za vitenge, sita za kanga kwenye maduka matatu tofauti eneo la Soko Kuu la Halmashauri ya Manispaa Songea.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Marco Chilya, aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Anna Mtete (22) mkazi wa kijiji cha Ndiwili mkoani Iringa, Adelaide Kihaka (62) mkazi wa kijiji cha Kidabaga, Kilolo mkoani Iringa na Grace Kihombo(42) mkazi wa Dar es Salaam. Chilya alisema watu hao walinaswa katika doria, misako na operesheni katika kipindi cha Septemba, mwaka huu, ambazo zilikuwa na mafanikio.

Alisema watu hao walikamatwa Oktoba 3, mwaka huu majira ya saa 5:00 asubuhi katika maeneo ya mtaa wa Sokoni Kata ya Mjini, Manispaa ya Songea na katika kijiji cha Mtyangimbole, Halmashauri ya Madaba wilayani Songea wakiwa na mali mbalimbali za wizi ambazo zinadaiwa waliiba katika maduka matatu tofauti Songea mjini.

Mbali na vitenge na kanga hizo, alisema watuhumiwa hao pia walikutwa na suruali 31 aina ya Cardet, pasi mbili za umeme, ndoo ndogo 10 za mafuta ya kupikia, ndoo moja yenye ujazo wa lita 20 ya mafuta ya kupikia na bidhaa mbalimbali za madukani.

Kwa mujibu wa Kamanda Chilya, watu hao walikamatwa wakiwa wanasafirisha kwenda mkoani Njombe kwa kutumia gari lenye namba za usajili T 576 EHV Toyota Haice mali ya Rioba Mapunda, mkazi wa Songea mjini.

Alisema siku hiyo ya tukio, watuhumiwa hao walifanya wizi huo kwa kutumia mbinu ya kuingia kwenye maduka kama wateja huku mmoja wao akifanya kazi ya kuwalaghai wauzaji kama wanahitaji kununua bidhaa na wengine wakiwa wanaiba kwenye maduka hayo.

Kamanda Chilya alisema Jeshi la Polisi mkoani hapa linafanya ufuatiliaji kwa kina ili kuubaini mtandao wote unaojihusisha na matukio hayo ya wizi kwa kutumia mbinu hizo huku kibainisha kuwa watuhumiwa wengine, kwa mujibu wa taarifa za kiintelejensia, wanadaiwa wako wilayani Mbinga wakiendelea na matukio ya wizi wa aina hiyo.

Wakati huo huo, Kamanda Chilya alisema kupitia operesheni mbalimbali zinazoendelea kufanyika katika maeneo yote mkoani Ruvuma, mamekamata kete 36 za bangi na kuteketeza shamba la bangi lenye ukubwa wa robo heka ambalo lilikuwa na miche 76 iliyochanganyika na mahindi yaliyokuwa yamelizunguka shamba.

Alisema watuhumiwa wawili wameshakamatwa na majina yao yamehifadhiwa kwa uchunguzi zaidi na baada ya kukamilika, watafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

# Simbachawene aonya ufujaji fedha za miradi

**Na Mwandishi Wetu,** BUNDA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amewataka viongozi mkoani Mara kutumia kwa uangalifu fedha za miradi ya maendeleo ili kukamilisha kwa ufasaha na kuepukana na hoja za ukaguzi.

Simbachawene alisema hayo juzi akiwa katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Mara ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kikazi ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kusikiliza changamoto za wananchi mkoani Mara.

Waziri Simbachawene aliwataka viongozi hao kuwa waaminifu katika utekelezaji wa miradi hiyo ya maendeleo.

Alisema miradi mikubwa ina changamoto nyingi kwani kila mmoja anatupia jicho kwenye miradi hiyo wakiwamo wafanyabiashara wa vifaa vya ujenzi kupandisha bei.

"Kwa kuwa mnatumia 'Force Account' katika ujenzi wa shule hii ya mkoa, mnatakiwa kuwa wabunifu. Mkiona wafanyabiashara wanapandisha bei vifaa vya ujenzi basi kanunueni kiwandani. Msije mkanunua bei ya juu na kujiingiza katika hoja za ukaguzi," alisema.

Katika kuhakikisha wanafunzi wa shule hiyo ya mkoa wanapata huduma ya elimu kikamilifu, Simbachawene aliwataka viongozi hao kuangalia namna ya kuanza ujenzi wa nyumba za walimu haraka iwezekanavyo.

"Shule nzuri namna hii ni lazima iwe na nyumba za walimu ili wanafunzi wapate huduma ya elimu kwa ufasaha, hivyo tafuteni namna ili nyumba za walimu zianze kujengwa haraka," alisema na kuongeza kuwa suala la ujenzi wa nyumba za watumishi halina budi kuwekewa mkakati ili kutekelezwa kwa ufasaha.

Katika hatua nyingine, Simbachawene aliwataka viongozi hao kutatua changamoto ya ukosefu wa maji katika Zahanati ya Nambaza ambayo aliweka jiwe la msingi.

Alisema ameshangazwa kwa kitendo cha zahanati hiyo kukosa huduma ya maji wakati imezungukwa na Ziwa Victoria.

"Nashindwa kuelewa sababu ya zahanati hii ambayo imezungukwa na Ziwa Victoria kukosa huduma ya maji. Haiingii akilini kwa kweli, hebu tafuteni namna ya kusogeza hayo maji katika eneo hili ili wananchi waweze kunufaika na uwepo wa zahanati hiyo na kwa shughuli zao za uzalishaji," alisema.

Simbachawene alihitimisha ziara yake ya kikazi ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuzungumza na wananchi katika mkoa wa Mara kwa kutembelea Halmashauri ya Wilaya ya Bunda na kuweka jiwe la msingi mradi wa Zahanati ya Nambaza, kuzindua Shule ya Sekondari ya Bunda Mjini, kukagua Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Mara na kuzungumza na wananchi wa Bunda.

# HABARI KATIKA PICHA




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa Huduma za Uhandisi Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Mhandisi Erick Madinda kuhusu ujenzi, upanuzi na ukarabati wa daraja na barabara ya Mivinjeni na Bandari One jijini Dar es Salaam, akiwa katika ziara ya kikazi wilayani Temeke, jana. Kulia ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dar es Salam, Abbas Mtemvu. **PICHA: OWM**



Ofisa Uhusiano na Masoko wa Kampuni ya Itel, Sophia Msafiri, akiwakabidhi mabegi wanafunzi wa Shule ya Msingi Tandale, katika hafla ya kukabidhi msaada wa vitu mbalimbali vilivyotolewa na kampuni hiyo, Kinondoni, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mwendesha baiskeli ya miguu mitatu maarufu guta, akiwa amelisheheni matairi na kumfanya ashindwe kuona nyuma katika Barabara ya Morogoro, eneo la Jangwani, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba (kushoto), akiwa na Balozi wa Hungary nchini, mwenye makazi yake jijini Nairobi, Kenya, Zsolt Mészáros baada ya kufanya mazungumzo, jijini Dar es Salaam jana. Dk. Nchemba, alitoa wito kwa wawekezaji kutoka Hungary kuja kuwekeza nchini katika maeneo mbalimbali watakayoona yanawafaa kutokana na serikali kuweka mazingira bora yanayovutia uwekezaji. **PICHA: WF**



Mmoja wa Wanachama wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT), Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, akichangia damu, wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Umoja huo, katika uwanja wa Tawi la Muungano, mjini Zanzibar jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# MAISHA

Oktoba 6, 2024

Nipashe


Baba, Mama na Mwana *Jumapili*




# Tumia bamia kumaliza chunusi

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | ■ | N | D | A | N | I |
| A | ■ | ■ | ■ | K | ■ | N |
| G | ■ | G | A | O | ■ | G |
| E | D | A | ■ | M | E | I |
| N | ■ | M | K | E | ■ | Z |
| D | ■ | B | ■ | ■ | ■ | W |
| O | B | A | M | A | ■ | A |

## AMSHA AKILI








## FUMBO TOTO

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | ■ | | | | | |
| | ■ | ■ | ■ | | ■ | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | | | ■ | | | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | ■ | | ■ | ■ | ■ | |
| | | | | | ■ | |

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

EDA, KUU, INA, DAU, RUNGU, IGANA, NYUKA, DAIMA, MAJESHI, UNGUZWA

## TOA TOFAUTI 5



## WATOTO

# PAKA RANGI







Alichokifanya daktari

Mama mmoja alikuwa anafanya usafi chumbani na ghafla aliona kisanduku chini ya uvungu wa kitanda cha mtoto wake.

Alipokifungua akakuta mawe madogo 15 yakiwa ndani, ndipo alipokwenda kumuuliza mtoto ake.

Mama: Kisanduku hiki cha nini?

Mtoto: Mama kisanduku kina mawe yangu

Mama: Ndiyo, haya mawe ya nini?

Mtoto: Mama nisamehe, hayo mae nilikuwa nayaweka kila nikiiba yai la kuku wako.

Mama: Wee mtoto yani umeshakula mayai 15, sasa nitakuadhibu

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Dalili hatima ya mtoto iliyopindishwa

KARIBU tena msomaji wangu katika safu yetu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki iliyopita nilisema kuzaa ni tofauti na malezi, na matunzo ni tofauti na kulea. Kulea ni kuongoza, kuelekeza na kumwandaa mtoto wako.

Aidha, aliyepewa jukumu la kulea ni mwanamke. Mwanamume halei bali anatoa matunzo. Pamoja na ukweli huo, je, wazazi hawa wanajua hatima ya mtoto au watoto inaweza kupindishwa?

Kila mtoto anazaliwa na hatima fulani. Hatima ni kile alichokusudiwa. Mtu anaweza kuzaliwa akiwa hana kitu chochote. Lakini katika ulimwengu wa roho amebebeshwa vitu vingi sana.

Wazazi wanaweza kufurahia watoto pasipo kujua wana nini, wamebeba kusudi gani! Lakini wanaweza kupindishwa badala ya kwenda hivyo wao wanakwenda tofauti.

Mungu katika moja ya maneno yake anasema "hata mtoto hujijulisha kwa matendo yake; kwamba kazi yake ni safi, kwamba ni adili" (Mithali 20:11).

Watoto huonyesha wao ni nani. Mungu anaweza kukuleta toka kule mwisho, akakutambulisha huku mwanzoni. Mambo anayofanya mtoto leo huonyesha atakuwa ni nani. Kuzimu huwa wanafuatilia hatima za watoto. Yesu inaelezwa alianza kushangaza watu akiwa na umri wa miaka 12. Hekima zake, maneno yake yalionyesha ni mtu wa ajabu.

Mtoto wa miaka ya leo anaweza kukuonyesha kwenye simu mambo ya ajabu ambayo mzazi hajawahi kujua. Mtoto anaweza kufanya vitu vya kiinjinia lakini akapuuzwa, kumbe hiyo ndio fani yake.

Wewe unaishi na watoto lakini kuzimu wanawajua. Mungu hakuumba watu waishi kimaskini. Huenda msomaji wangu ulipindishwa hatima tangu ukiwa mdogo.

Fikiria ulivyokuwa mdogo, ulivyokuwa na akili darasani. Kumbe wako watu wabaya walishakumaliza tokea ukiwa mtoto. Watoto unaowaona leo, ndio matunda yako, ndio watakaotangaza lako baadaye!

Swali ni je, utajuaje hatima ya mwanao imepindishwa? Hebu tafakari dalili zifuatazo;- Kwanza, tokea mimba ni matatizo. Ukiona hivyo, fahamu ya kuwa huyo uliombeba siyo wa kawaida.

Dalili nyingine hatima kupindishwa ni pale mtoto anapozaliwa tu na wanazazi wake wakafa. Ukiona hivyo, mtoto huyo siyo wa kawaida.

Mtoto anayezaliwa kisha uchumi wa baba ukaanguka. Huyo mtoto anaweza kuwa na hatima yake. Baba au mama walevi wanamtupa mtoto, fahamu ya kuwa huyo siyo wa kawaida.

Vile vile angalia mtoto anafuatwa na watu wa aina gani. Angalia pia aina za marafiki wanaomfuata. Kama mtoto rehema za Mungu hazijamfunika, aweza kupindishwa hatima yake. Magonjwa mengine hutumwa kwa mtoto ili kupindisha hatima yake.

Msomaji wangu, baada ya kuangalia dalili, hebu sasa tuone jinsi hatima inavyopindishwa. Ukiona mama anamnywesha pombe mtoto wake, hiyo maana yake anamkabidhi kwa mapepo.

Wako wanaume wanataka utajiri, wanawatoa sadaka watoto wao kwa njia ya kafara. Mtoto anaweza kuwa ameshauzwa na wanafanya hivyo ili wapate divai au fedha!

Huenda wazazi, mababu hawakujua zama hizo, siyo wacha Mungu, matokeo yake leo mtoto amekuwa hovyo, mlevi, kumbe pombe ulipewa ukiwa mtoto.

Maandiko ya Mungu yanasema, kile unachopanda ndicho utakachovuna, ukipanda mchicha utavuna mchicha huo huo na siyo maharage. Hiyo ni kanuni!

Wako baadhi ya wazazi hutumwa vitu fulani kutoka kwa watoto wao na kuwapelekea waganga wa kienyeji. Umaskini tunaupatia duniani.

Kitu kingine ni kwamba ibilisi anaweza kuwaleta wanao watu wasiokuwa sahihi. Mzazi inapaswa ukae karibu na mwanao, msaidie, mlee akue!

Fuatilia hata ndoto za watoto wako. Wengine tayari wanatumiwa na wachawi. Usipomweka wakfu mwanao, kuzimu watafanya hivyo.

***Wazazi wengi wanachojua ni kutoa hela na kumpa mtoto aende shule, wala humsaidii. Neno la Mungu linasema, "Mwenye kusimamia nyumba yake vema ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi

# Msiwahukumu, wapeni somo miradi inalipa

HAYATI Mzee Reginald Mengi, aliyewahi kuwagusa mamia kwa makumi, ndani na nje ya nchi kwa wema wake, utu na kujali shida za watu wengine aliwahi kusema: "Usichoke kusaidia wanaotaka msaada wako. Jiulize ungekuwa wapi leo kama Mungu angechoka kukusaidia."

Ndugu zangu, nimelazimika kuanza na nukuu hiyo ya aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa Kampuni za IPP na mfanyabiashara tajiri aliyeacha alama na kumbukumbu katika vichwa vya Watanzania wengi.

Wako wanaharakati wanasema katika maisha usipopambana tabia ya kuomba inadhalilisha. Wanasahau kuna watu wanatajwa katika vitabu vitakatifu vya dini kwamba wanahitaji msaada.

Tunao mitaani hata kama wako ambao wamejivisha kilemba cha wanaotajwa na mitume wa Mwenyenzi Mungu.

Kibaya zaidi kuomba inakuwa aibu ya kwanza, kunyimwa unachotaka inakuwa aibu ya pili na kutangazwa inakuwa aibu ya tatu. Hii inatufundisha nini, pambana sana kutafuta fedha, maana umasikini unadhalilisha mno.

Ulemavu hujumuisha walio na changamoto za kimwili, kiakili na kihisia za muda mrefu, ambazo zinapoingiliana na vikwazo vya kimitazamo, kimazingira na kitaasisi, hufanya iwe vigumu kwao kushiriki kikamilifu na kwa ufanisi katika shughuli za jamii sawa sawa na wengine.

Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya Mwaka 2010 kwa Tanzania Bara na Sheria ya Watu wenye Ulemavu (Haki na Fursa) ya Mwaka 2006 kwa Zanzibar, zote zinawatambua wenye ulemavu na kuwaweka kwenye mipango ya huduma mbalimbali. Haijalishi mahali wanakoishi au jinsi zao.

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuhusu uwezeshaji kwa jamii ya watu wenye ulemavu, inaonyesha kuwa kwa mwaka 2022/23/24, watu wenye ulemavu waliotambuliwa walikuwa 154,844. Kati yao wanawake ni 76,178 na wanaume ni 78,666. Hao ni wale ambao walitambuliwa na kufanyiwa tathmini.

Licha ya kutambuliwa na kufanyiwa tathmini, pia walipewa huduma za mahitaji mbalimbali. Pamoja na kuwapo jitihada mbalimbali za kuwainua kiuchumi, watu wenye ulemavu wanapata ukosefu wa ajira mara mbili ya kiwango cha wale wasio na ulemavu.

Sijui unanielewa? Hisani iepuuza njia ambazo sera na mifumo iliyopo inawatenga na au kuwaadhibu wenye ulemavu na kuwanyima usalama wa kiuchumi. Ni wazi kwamba, ufadhili hauwezi kuendeleza haki ya kiuchumi bila ya kujumuisha lenzi ya ulemavu.

Tuwape nafasi katika miradi ya kiuchumi, na serikali ijikite zaidi kuhusianisha sera na mipango na uwezeshaji kiuchumi ili kuwaondoa jamii hii katika utegemezi wa kipato.

Huko mitaani, mijini na hasa katikati ya mji na vituo vya mabasi, kuna idadi kubwa ya watoto, vijana na wazee wanaozunguka kutwa nzima wakiomba pesa. Hakuna anayewaona na kutafuta ufumbuzi wa kuwaondoa mitaani, ili kuacha kuombaomba pesa kila uchao.

Mbona halmashauri zetu zikijipanga wanaweza kujenga mwitikio wa pamoja wa kuwajumuisha kupata miradi katika sekta mbalimbali.

Pasina shaka watu wenye ulemavu wanapata changamoto kupata maeneo ya kufanyia shughuli za uzalishaji mali, kama kwenye masoko ya walaji lakini haizuii wao kupambana kutafuta na kuvuja jasho ili kukuza uchumi wao.

Wenye ulemavu wanaweza kujinasua huko kwa kujipa maono kwamba kuanzia sasa hatutaki ombaomba, tunataka kazi.

Kwa kuwa ugumu wa maisha, ndio kipimo cha akili, basi kazi itamwezesha kujitegemea na kupata heshima katika jamii.

Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2010, Ibara ya 33, Ibara ndogo ya tatu, inasema kila mwajiri anaeweza kuajiri watu 20 ni lazima asilimia tatu, wawe watu wenye ulemavu na atengeneze miundombinu itakayowawezesha kufanya kazi.

Pamoja na kuwepo kwa sheria hiyo, mbona bado kuna baadhi ya waajiri hawafuati utaratibu huo, ili kupunguza idadi ya wanaoombaomba mitaani, stendi?

Zile asilimia mbili za mikopo isiyo na riba, inayotolewa na kila Halmashauri kutokana na makusanyo ya mapato ya ndani; tumejiridhisha kwa kiasi gani zimewainua kiuchumi wenye ulemavu?

Iko wapi ripoti ya tathmini ya namna walivyopiga hatua moja kiuchumi au tunafanya siasa?

Kongole kwa Idara ya Sera na Mipango, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu kwa kuamua kuja na mapitio ya Sera ya Taifa ya Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2004 ili iendane na mazingira ya sasa.

Kwenye suala la ajira, wamekuwa wakibaguliwa jambo ambalo limekuwa likiwaathili kisaikolojia. Kwa namna iwayo yote ile, serikali imeweka kipaumbele kutoa nafasi za ajira kwa watu wenye ulemavu, ambao wanakidhi vigezo na wenye sifa.

Kutokana na hali hiyo, serikali imeweka msisitizo kwa mwombaji kujieleza uleumavu alionao, ili kurahisisha uchambuaji wa maombi ya kazi, lakini suala hili bado limekosa uwazi na kusababisha changamoto kwa baadhi ya waombaji kukosa nafasi.

• ***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***



# MITINDO

Na Moshi Lusonzo

# TUPIA MACKENZIE UPATE FURAHA



VAZI la Mackenzie linaendelea kutamba katika bara la Afrika. Wanaume kwa wanawake wanapenda kuvaa nguo hizi zenye mwonekano halisi wa Kiafrika.

Kwa ujumla vazi la Mackenzie linatengenezwa kwa kitambaa chenye rangi mchanganyiko na kutoa mwonekano wa kupendeza zaidi.

Wataalamu wa masuala ya mavazi wanasema, nguo aina ya mackenzie ina asili ya Wamarekani weusi, lakini limesambaa katika nchi mbalimbali duniani.

Kwa upande wa Tanzania, watu wa rika na jinsia tofauti wanavaa vazi hili, na kwa kupitia wabunifu kuna mitindo mbalimbali inayovutia.

GAUNI

Inapendeza sana kwa kushona gauni la moja kwa moja; nguo hii inamfanya mwanamke kuonekana kama amevaa dila lenye maua mchanuo, kweli mvaaji anatoka bomba sana.



**SHATI NA SKETI**

Mackenzie inampa mvaaji mvuto wa aina yake pale anaposhona shati na sketi au suruali. Unachotakiwa kufanya kuhakikisha marembo yanawekwa katika mpangilio mzuri.


GAUNI MCHANGANYIKO.

Baadhi ya watu wanashona gauni la Mackenzie kwa kuchanganya na vitambaa tofauti.

Hilo halitoi maana ya vazi hili, bali linazidisha nakshi na kumfanya mtu kupendeza zaidi.

**VIKOI VYA MACKENZIE**

Kama vile haitoshi, unaweza kushona vikoi vya Mackenzie bila ya kuwa na wasiwasi. Mwanamama anayevaa gauni linalotokana na vikoi hana sababu ya kuchukia kwani inampa nafasi ya kutembea kwa madaha na furaha kwa sababu linamng'arisha sana.



UREMBO

Na Mary Geofrey

# Tumia bamia kumaliza chunusi



SUALA la urembo lina eneo pana linalohitaji umakini mkubwa kwa sababu ndio mwanzo wa mwonekano wa mwanamke kabla ya mavazi.

Urembo unaweza kukufanya ukaongeza thamani yako au ukaishusha.

Mara nyingi tumezoea kuona watu wenye chunusi wakitumia vipodozi vyenye kemikali kuondoa ilihali kuna njia za asili za kumaliza tatizo hilo kabisa.

Unaweza kutumia bamia ambayo ni mboga ikipikwa lakini ukabadilisha matumizi yake ni kipodozi cha kuondoa chunusi.

Bamia inatibu chunusi na kuziondoa moja kwa moja. Mbali na chunusi, pia husababisha ngozi kuteleza na kuwa nyororo.

Namna ya kutumia

Chukua bamia zikatekate vipande, ziweke kwenye brenda kisha chukua limao kipande na maji kidogo, weka kwenye brenda kisha saga.

Baada ya kupata mchanganyiko wako upake usoni mpaka kwenye shingo, acha kwa muda likauke kisha bandua kama unavyoondoa maski nyingine usoni.

Rudia hivyo mara tatu kwa wiki itasaidia kuondoa kama si kumaliza kabisa tatizo la chunusi.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Namna ya kutengeneza visheti



VISHETI ni aina ya kichangamsha kinywa ambacho unaweza kula na kinywaji kama na kahawa, chai, juisi na maji.

Visheti unaweza kutengeneza nyumbani kwako kwa njia rahisi na muda mfupi.

**MAHITAJI**

Unga vikombe viwili, samli au shortening ya mboga vijiko vya supu viwili, maziwa robo tatu ya kikombe, iliki kiasi na mafuta kisi ya kukaangia.

Mahitaji ya shira ni sukari kikombe kimoja, maji robo tatu ya kikombe, vanila kikombe na zafarani (ukipenda) nusu kijiko cha chai.

**JINSI YA KUPIKA**

Katika sufuria pasha moto maziwa na wakati huo huo chemsha samli katika sufuria nyingine.

Tia unga katika bakuli na iliki, kisha mimina samli iliyochemka na huku unachanganya.

Weka maziwa na uendele kuchanganya vizuri isiwe na madonge, ikiwa maziwa hayatoshi ongeza maji kidogo.

Kisha uache unga ukae mahali pa joto kwa muda wa dakika 10.

Halafu fanya viduara vidogo vidogo, kisha finyiza kwenye greta yenye vishimo vidogo ili upate umbo lake.

Kisha kaanga kwenye mafuta yaliyopata moto hadi vibadilike rangi ya dhahabu, kisha viepue vichuje mafuta.

Chemsha shira, ikiwa tayari mimina visheti na upepete na kuzichanganya zipate shira kote.

Weka kwenye sahani na zitakuwa tayari kwa kuliwa na kahawa.

## Tumia michoro ya ramani kutengeneza bustani



**Na Restuta James**

UTENGENEZAJI wa bustani nyumbani au hata sehemu ya kazi unaboresha na kupendeza mazingira na hili limefanyika kwa karne zote.

Hata hivyo, ubunifu umeongeza mpangilio wa kujenga mistari ya mawe (kerbstones) na vigae vya tofali za ardhini (paving blocks), kama ardhi ngumu pamoja na upandaji miti kwa mpangilio sahihi ili kuongeza mvuto na thamani ya nyumba na mandhari yake kwa kiasi kikubwa.

Mtaalamu wa bustani, Daisy Msigwa, anasema pamoja na kwamba ukisasa umeingia kila sekta, suala la mazingira lina mchanganyiko wa ukale na ukisasa, unaotengeneza mandhari nzuri zaidi.

Anasema mandhari inayozunguka nyumba inajumuisha ardhi iliyopandwa maua, miti na nyasi kwa ajili ya kupumzika na sehemu ya paving kwa ajili ya kutembea kwa miguu au gari.

"Pamoja na maua, tunashauri na kusisitiza umuhimu wa kupanda si tu miti ya kivuli, bali ile ya matunda na eneo la mboga. Eneo lenye kijani kibichi linapaswa kuwa kubwa zaidi nyumbani kwa ajili ya hewa na kupumzisha ubongo," anasema.

Anasema wako wanaopenda maji (water landscape) ambayo hujumuisha bwawa la kuogelea, la samaki, mifereji ya umwagiliaji na maji yanayoruka, akishauri watumie wataalamu hasa kwa familia zenye watoto wadogo.

"Haya yote yakiweka katika mpangilio sahihi kwenye eneo la kiwanja linalozunguka nyumba huongeza sana thamani ya makazi," anasema.

Anasema ili mpangilio uwe na uwiano, ni muhimu yote yakazingatia michoro ya ramani kabla ya utekelezaji. "Unapotanguliza utekelezaji bila ya michoro ya ramani ya bustani na mandhari yote ya nyumba pamoja na mahusiano yake na nyumba yenyewe, unajiandaa kukutana na tatizo kubwa hasa ubora wa kazi utakuwa wa viwango vya chini," anafafanua.

**Na Elizabeth Zaya**



# KIPAMBE CHUMBA CHAKO KIVUTIE

SEHEMU au chumba kinachotumika kuvalia nguo (dressing room) ni muhimu na ndipo mahali pekee ambapo huchangia kumtoa mtu akiwa amependeza au amechukiza.

Watu wengi wanaokuwa wamependeza wanapotoka ndani na kuvutia machoni mwa watu ikiwamo kusifiwa kwamba wamependeza, siri yake huwa ni chumba maalum ambacho hutumika kuvalia.

Kwa hiyo kutokana na umuhimu huo, leo nataka nizungumzie umuhimu wa kutunza chumba hiki.

Kutokana na umuhimu wake, kuna haja kubwa kuhakikisha kinawekwa katika mazingira mazuri ya kuvutia kama ambavyo watu wanaokitumia hutoka humo wakiwa wamependeza na kusifiwa na watu.

Baadhi ya vitu vya kuzingatia katika kuhakikisha chumba chako kinakuwa katika mvuto ni pamoja namna ya kupangilia vitu vinavyowekwa kwenye chumba chako hicho.

Kwa mfano kabati, sitazungumzia kwa ndani vitu vinavyotakiwa kuwamo isipokuwa nataka nioneshe baadhi tu ya vitu na namna unavyoweza kupangilia chumba hicho.

Katika mpangilio wa kabati unapaswa kuangalia sehemu sahihi ya kuweka kabati lako hilo, liwe la ukutani au kusimama kawaida.

Katika eneo hili ni muhimu kuwa makini kwa sababu ukifanya makosa kuliweka katika mwelekeo sahihi kuna hatari kubwa ya kuharibu mwonekano wa chumba chako na hata usifurahie uwapo wa kabati lenyewe na pia likakumalizia nafasi au likawa ni eneo ambalo halionyeshi mwanga mzuri.

Kwa hiyo, baada ya kuliweka katika eneo sahihi, tupia macho kwenye eneo jingine tena, kwa mfano sehemu ya kupangilia begi ndogo za mkononi, hakikisha napo hapa panapangiliwa vizuri, kama umezining'iniza, hakikisha ni zile ambazo zinatumika tu, nyingine ambazo huna kazi nazo usizirundike humo chumbani.

Kadhalika, eneo la kuwekea viatu, nalo lipangilie vizuri, hakikisha vinavyohifadhiwa chumbani ni visafi.

Kwa ujumla wake, ninachozungumzia hapa ni kuweka ubunifu katika mpangilio wa chumba chako, kwamba kila kitu kilichoko ndani ya nyumba au chumba chako kiwekwe katika utaratibu mzuri, usiweke vitu vyako ilimradi bali kwa kuzingatia vyote vinatumika kuleta mvuto wa chumba bila kujali ni vya dizaini gani.

Lengo ni kuweka nyumba yako katika hali ya usafi na yenye kuvutia, isiyochosha macho wakati wote, katika kila eneo la nyumba yako.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO -
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
ULIKUWA UNAPIGANA AU ULISIMAMA TU ULINGONI?
SIJASIMAMA ILA ALINIKUMBUKA NILIMTUKANA BAR.
ULIPOMKUTA MKEO NA MGONI WAKO ULICHUKUA HATUA GANI?
'NILIZIMIA'
MWAKA HUU NAGOMBEA.
BADO UNAGOMBEA HAWALA?
OYA! BRO ULIAHIDI UTATUKOMBOA!
ULISIKIA VIBAYA
BOB VIPI MBONA KAMA UMENIKAUSHIA
NINI CHIPSI AU?

# Chanjo ya Mpox yaanza kutolewa Goma

**KINSHASA, DRC**

WAZIRI wa Afya wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Samuel-Roger Kamba, amesema chanjo ya kwanza dhidi ya mpox imeanza kusambazwa katika kitovu cha janga hilo huko Goma, katika mkoa wa Kivu Kaskazini.

Waziri huyo aliyasema hayo katika mkutano na waandishi wa habari katika mji mkuu wa Kinshasa, akieleza kuwa chanjo dhidi ya virusi hivyo ilipangwa kuanza kutolewa Jumatano.

Alisema chanjo hiyo ilicheleweshwa haswa kutokana na kucheleweshwa kwa utoaji wa dozi kupitia nchi za Afrika ya Kati ambazo ni kubwa mara nne ya Ufaransa.

Kwa mujibu wa Kamba, chanjo za kwanza zitatolewa huko Goma, mji mkuu wa mkoa wa Kivu Kaskazini, kwa makundi ya watu wanaoonekana kuwa hatarini zaidi kama vile wafanyakazi wa afya, watu wanaowasiliana nao na wagonjwa.

Mashariki mwa DRC ndio eneo lililoathiriwa zaidi na virusi, ikielezwa kuwa ujumla nchi hiyo imerekodi zaidi ya wagonjwa 30,000 na karibu vifo 990 tangu kuanza kwa mwaka na vifo vingi kati ya watoto.

"Takriban asilimia 70 ya vifo vinahusu watoto walio chini ya umri wa miaka mitano, licha ya kuwa chanjo hiyo inahusu watu wazima tu katika hatua hii.

Alisema DRC ilipokea dozi 265,000 mwezi uliopita zilizotolewa na Umoja wa Ulaya na Marekani, na kwamba chanjo hiyo iliyotengenezwa na maabara ya Denmark ya Bavarian Nordic, imekusudiwa watu wazima pekee.

Ilielezwa kuwa chanjo nyingine dhidi ya Mpox, ambayo inaweza kutolewa kwa watoto, imeidhinishwa na Japan, ambayo DRC iko katika majadiliano juu ya usambazaji unaowezekana.

"Mahitaji ni makubwa zaidi, unaweza kufikiria kuwa katika nchi yenye wakazi milioni 100, sio kwa dozi 265,000 ambazo tunatatua shida.

"Tunasubiri kundi la pili la chanjo za Bavaria Nordic ambazo zilitangazwa kwetu na Ufaransa, za dozi 100,000, kuwasili lakini tunasubiri zaidi dozi milioni tatu ambazo Japan imeahidi," alisema Kamba.

Vile vile, ilielezwa kuwa nchi hiyo lazima pia ipate vipimo 4,500 vya uchunguzi wa mapema ili kukabiliana vyema na janga hilo kwa matibabu na utunzaji wa haraka.

Shirika la Afya Duniani (WHO) lilitangaza Ijumaa kuwa limeidhinisha kipimo cha PCR ili kugundua DNA ya virusi na swabs kutoka kwa vidonda vya ngozi.

Ilielezwa kuibuka tena kwa kesi mpya kumesukuma WHO kuanzisha kiwango chake cha juu zaidi cha tahadhari ya kimataifa mwezi Agosti.

Virusi hivyo vipo katika nchi 16 za Afrika, kwa mujibu wa kituo cha kudhibiti magonjwa cha Umoja wa Afrika (Africa CDC).

**RFI**

# Marekani yazishambulia ngome 15 za Wahouthi

**WASHINGTON,** MAREKANI

JESHI la Marekani limesema vikosi vyake vimefanya mashambulizi katika maeneo 15 ya ngome zinazodhibitiwa na wanamgambo wa itikadi kali Wahouthi huko Yemen kwa lengo la kufifisha uwezo wao wa kushambulia meli.

Kwa mujibu wa televisheni ya wanamgambo wa Houthi Al Masirah, mashambulizi hayo yamelenga maeneo manne tu kati ya 15 yaliyoelekezwa shabaha.

Ilielezwa kuwa Marekani na Uingereza zimekuwa zikifanya mashambulizi yenye lengo la kuusitisha uwezo wa Wahouthi kuzishambulia meli, ila mashambulizi ya waasi hao kwenye meli zinazopitia Bahari ya Shamu na Ghuba ya Aden, yameendelea.

"Kamandi Kuu ya Marekani (CENTCOM) imefanya mashambulizi ikilenga ngome 15 za Wahouthi katika maeneo yanayodhibitiwa na Wahouthi nchini Yemen," ilisema kamandi hiyo katika ujumbe wake kwenye mtandao wa kijamii.

Televisheni ya Al Masirah iliyosema Marekani na Uingereza zote ziliishambulia Yemen Ijumaa, awali ilikuwa imeripoti mashambulizi manne huko Sanaa na mengine saba Hodeida, huku waandishi wa shirika la habari la Ufaransa AFP, wakisema walisikia milipuko mikubwa katika hiyo miji yote miwili.

Wahouthi wanaoungwa mkono na Iran wamekuwa wakizishambulia meli katika njia hiyo tangu mwezi Novemba wakidai lengo lao ni meli zilizo na mafungamano na Israel na mashambulizi hayo yanalenga kuonyesha mshikamano na Wapalestina wakati wa vita vya Israel dhidi ya Hamas huko Gaza.

Wakati hayo yakiendelea, ilielezwa kuwa Israel pia imeishambulia Yemen kutokana na hayo mashambulizi ya Wahouthi. Hata hivyo, ilielezwa kuwa mashambulizi ya Israel huko Hodeida mwezi uliopita yalisababisha vifo vya watu watano baada ya waasi hao kusema kwamba waliulenga kwa kombora uwanja wa ndege wa Ben Guiron nchini Israel.

**DW**



Moshi mzito ukionekana kutanda juu ya makazi ya watu baada ya shambulio la anga la Israel nchini Lebanon ambako raia zaidi ya 600 wameuawa juzi. **PICHA: MTANDAO.**

# Wafanyakazi wa Kiafrika wafungiwa majumbani Lebanon

**BEIRUT,** LEBANON

UMOJA wa Mataifa (UN) umesema wafanyakazi wa nyumbani ambao ni Waafrika huko nchini Lebanon wamefungiwa majumbani huku waajiri wao wakikimbia mashambulizi ya anga ya Israel.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Uhamiaji (IOM) lilisema jana kuwa wafanyakazi wa ndani wa kigeni wanazidi kutelekezwa ili kukabili hatari kubwa katika mzozo huo.

Shirika hilo la IOM liliibua masaibu ya wafanyakazi wahamiaji 170,000 wa Lebanon, wengi wao wakiwa ni wanawake kutoka nchi kama Ethiopia, Kenya, Sri Lanka, Sudan, Bangladesh na Ufilipino.

"Tunapokea ripoti zinazoongezeka za wafanyakazi wa nyumbani wahamiaji kutelekezwa na waajiri wao wa Lebanon, ama kuachwa mitaani au majumbani mwao huku waajiri wao wakikimbia," alisema Mathieu Luciano, mkuu wa ofisi ya IOM nchini Lebanon. Aliongeza kuwa wahamiaji wanaotafuta msaada wanakabiliwa na chaguo finyu sana la makazi, na kwamba Alhamisi alitembelea makazi katika mji mkuu unaohifadhi familia 64 za Sudan ambazo hazina mahali pengine pa kwenda.

Alisema Shirika la IOM lilikuwa likipokea maombi yanayoongezeka kutoka kwa wahamiaji wanaotafuta usaidizi wa kurejea nyumbani, akieleza kuwa balozi nyingi pia zimeomba usaidizi wa shirika hilo kuwahamisha raia.

Hata hivyo, mkuu wa IOM alisema maombi hayo yangehitaji ufadhili mkubwa ambao hawana kwa sasa.

Ilielezwa kuwa takriban mwaka mmoja tangu ianze vita vyake dhidi ya Gaza, Israeli sasa imeelekeza mashambulizi yake Lebanon na kusababisha maelfu ya wananchi kukimbia makazi yao.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya ya Lebanon mashambulizi ya Israel nchini humo yameua zaidi ya watu 1,000 tangu Septemba 23, huku maelfu wakikimbia makazi yao katika nchi ambayo tayari imekumbwa na mzozo wa kiuchumi.

Wakati hayo yakiendelea, ilielezwa kuwa hali ya wafanyakazi wahamiaji wa Lebanon ni hatari, kutokana na kwamba hali yao ya kisheria mara nyingi inahusishwa na mwajiri wao.

"Tumeona huko kusini waajiri wangeondoka lakini wangewaacha wafanyakazi wa ndani mitaani, wasihame nao au mbaya zaidi, wanamfungia mfanyakazi wa ndani, kuhakikisha kuwa nyumba iko na kuhifadhiwa wakati wanatafuta usalama mahali pengine," alisema. Luciano alisema wale walioachwa barabarani wangetatizika kuhama au kupata usalama, wakati wengi hawawezi kuzungumza Kiarabu.

"Wengi hawana hati. Hawana karatasi. Matokeo yake, wanasitasita kutafuta usaidizi wa kibinadamu kwa sababu wanahofia kuwa watakamatwa na wanaweza kufukuzwa," alisema.

Luciano alibaini kuwa kulikuwa na masuala makubwa kuhusu afya ya akili kati ya wafanyikazi wa nyumbani wahamiaji wanaofanya kazi nchini Lebanon.

**TRT**

# Msimamizi atoa maelekezo muhimu uchaguzi mitaa

**Na Rose Jacob,** ILEMELA

MSIMAMIZI wa Uchaguzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Ummy Wayayu, ametangaza maelekezo muhimu na ratiba ya uchaguzi wa serikali za mitaa, utakaofanyika Novemba, mwaka huu.

Wayayu alitoa maelekezo hayo katika mkutano uliofanyika juzi wilayani hapa akisema maelekezo hayo yanatoa mwongozo kwa wapigakura na wagombea kuhakikisha taratibu zote zinafuatwa.

"Maelekezo hayo yanatolewa siku 62 kabla ya uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni ya 9 ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa, kulingana na Tangazo la Serikali Na. 574 la Julai 12, 2024," alisema.

Aidha, Wayayu alisema mchakato huo unalenga kufanikisha uchaguzi wa uwazi, haki na usawa hivyo zoezi la kuandikisha wapigakura litafanyika kuanzia Oktoba 11 hadi 20, mwaka huu.

Alieleza mambo ya kuzingatia ni kwamba uchaguzi utafanyika Novemba 27, 2024, wapigakura ambao ni wakazi wa Ilemela wanatakiwa kujisajili au kujiandikisha kuanzia Oktoba 11 hadi 20, mwaka huu.

Pia alisema wagombea watachukua fomu kuanzia Novemba Mosi hadi 7 wakati uteuzi utafanyika Novemba 8. Muda wa kuweka mapingamizi ya uteuzi wa mgombea ni Novemba 8 hadi 9 na uamuzi utatolewa kuanzia Novemba 9 hadi 10.

"Rufani dhidi ya uamuzi kuhusu mapingamizi ya uteuzi, zitapokelewa, kuanzia Novemba 10 hadi 13,2024 na kamati ya rufani itatoa uamuzi kuanzia, Novemba 10 hadi 13, mwaka huu.

"Kmpeni zitaanza Novemba 20 hadi 26, 2024 saa 2:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni, hivyo wakazi wa Manispaa ya Ilemela wenye umri wa miaka 18 na kuendelea kushiriki katika uchaguzi, pamoja na kutambua umuhimu wa kujiandikisha na kupiga kura," alisema Wayayu.

Aidha, viongozi wa dini na vyama vya siasa walikumbusha jamii umuhimu wa kuchagua viongozi wenye sifa bora pia wawahimiza umma kujitokeza kwa wingi, ili kuchagua viongozi wenye maono ya maendeleo.

"Wananchi tujitokeze, kujiandikisha kwa wingi na siku ya kupiga kura pia tujitokeze kuchagua viongozi wanaostahili kutuongoza, wenye maono ya kulipeleka taifa mbele," alisema Sheikh wa Wilaya ya Ilemela, Abdulwarith Juma.

Mwenyekiti Mwenza wa Kamati ya Amani ya Viongozi wa Dini Wilaya ya Ilemela, Mchungaji Canon Mlugu, alitoa wito kwa wananchi kuzingatia sifa za wagombea badala ya ushabiki wa kisiasa, huku akisisitiza amani katika uchaguzi.

Kaimu Katibu wa Chama Cha Kijamii (CCK) Wilaya ya Ilemela, Holela Mabula, alisema ushirikishwaji umefanywa awamu kwa awamu kuhusu umuhimu wa kuielewa kanuni za uchaguzi ili kushiriki kwa ufanisi.

"Wananchi wajitokeze na sisi viongozi wa vyama ikitokea changamoto tutawajulisha. Tumejipanga kusoma na kuzielewa kanuni za uchaguzi tulizozipokea leo, tutakwenda kuzifanyia kazi na itakapotokea mambo kwenda tofauti na kanuni, tutapaza sauti zetu kuwajulisha wananchi," alisema.

# Serikali kuandaa mwongozo motisha kwa walimu

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI kwa kushirikiana na wadau imeandaa mwongozo wa utoaji motisha kwa walimu ili kuhakikisha wanapewa hadhi wanaostahili.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari na walimu wa Halmashauri ya Mji Njombe wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Walimu Duniani.

Prof. Mkenda alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 toleo la 2023 ambayo pamoja na mambo mengine, imesisitiza walimu kupewa hadhi na motisha stahiki ili wafanye kazi katika mazingira rafiki na wezeshi.

"Andiko hilo lipo katika hatua za mwisho na litasambazwa hivi karibuni. Aidha serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi ya walimu kujiendeleza ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi," alisema.

Prof. Mkenda alisema hatua hizo zitachochea utekelezaji wa elimu ya usawa na ujumuishi kwa kutambua utofauti wa kila mtoto katika ujifunzaji na ufundishaji.

"Nia ya serikali ni kuona walimu wetu wanafanya kazi katika mazingira rafiki na wezeshi kitaaluma na kimaisha kwa ujumla," alisema.

Waziri huyo alisema wakati wakisherehekea Siku ya Walimu Duniani, wanaomba wazazi, jamii na wadau wote kutambua jukumu lao muhimu katika kuchochea maendeleo ya elimu.

"Kwa umoja wetu tuendelee kuboresha mazingira yetu ya kazi na hadhi ya walimu wetu. Leo (juzi) naomba tusimame pamoja kuunga mkono haki zao, ustawi na maendeleo yao kitaaluma ili kuhakikisha kwamba walimu wetu wanamotisha ya kutosha kuwapa nguvu na hali ya kuendelea na kazi zao kwa umahili na ufanisi mkubwa," alisema Prof. Mkenda.

Naye Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omary, aliwataka walimu kuendelea kushikamana kwa sababu mazingira yao ya kazi yanahitaji zaidi umoja.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Magufuli, Deustelasta Mtewele, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwapandisha madaraja kwa sababu walikuwa hawapandi muda mrefu na kwa maboresho makubwa katika sera na mitaala.

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Ndoa imevunjika, bibi harusi kakimbilia Gabon



**Na Adam Fungamwango**

**Tumeshawahi kuona hata baadhi ya maharusi wakiwakataa wenzao siku ya ya harusi mbele ya padri, kasisi, mchungaji anayefungisha ndoa, huku umati wa ndugu, jamaa marafiki na wageni waalikwa wakishuhudia.**

KUNA mambo ya kushangaza sana duniani. Hebu fikiria, mtu na mpenzi wake wanafikia hatua ya kuoana. Wanatambulishana kwa wazazi, ndugu jamaa na marafiki.

Lakini siku ya harusi au siku ya kufunga ndoa, mmoja haonekani. Mmoja haendi kanisani, wala nyumbani wanapofunga ndoa. Unasikia bibi harusi au bwana harusi hakuonekana. Inaanza kushangaa tatizo ni nini?

Kama hakutaka kuoa au kuolewa kwa nini asiseme mapema wakati wa machakato mzima wa sherehe za harusi na ndoa? Kulikuwa na tatizo gani kutomwambia mwenzio asihangaike kualika watu ili aendelee na shughuli zake zingine.

Haya mambo wala si ya kufikirika. Yametokea sana huko nyuma na mifano ni mingi. Yanaendelea na yataendelea kwa sababu siku zote waswahili wanasema moyo wa mtu ni kichaka. Huwezi kujua lililomo ndani ya moyo wa mtu.

Mshangao mwingine mkubwa ni kwamba hata wenyewe wanaofanya vitendo hivyo wanakuwa wamealika ndugu zao, jamaa na marafiki kutoka sehemu mbalimbali, mfano unaweza kukuta hata harusi inafungiwa kwao, lakini akatimua tu na kwenda kusikojulikana.

Tumeshawahi kuona hata baadhi ya maharusi wakiwakataa wenzao siku ya ya harusi mbele ya padri, kasisi, mchungaji anayefungisha ndoa, huku umati wa ndugu, jamaa marafiki na wageni waalikwa wakishuhudia.

Mpaka sasa huwa haijulikani kwa nini huwa inatokea vile. Ni kuchanyikiwa? Hakupenda kuoa au kuolewa au vipi? Sasa kama mtu hapendi kwa nini asiseme mapema? Wengine wanahusisha mambo hayo na imani za kishirikina.

Wanadai inaweza kutokea kama mmoja wapo alimuacha mpenzi wake wa kwanza aliyeahidiana naye kufunga ndoa katika mazingira ya kutatanisha.

Inadaiwa kuwa kuna wakati wanaoachwa huwa hawaachi salama waliowakwaza.

Kutokana na matukio haya kujitokeza mara kwa mara, ndiyo maana kuna baadhi ya maharusi wanaanza kufunga ndoa kwa siri kabla ya sherehe za harusi. Wanadai inaondoa husuda na macho ya watu ambao si wazuri, pamoja na wabaya wao.

Wanamuziki wa dansi wameshatunga nyimbo na kuimba kuhusu matukio haya.

Kuna bi harusi mmoja alitoweka akiwa chumbani akipambwa kabla ya kuolewa. Tena alikuwa nyumbani kwao. Bwana harusi alipokuja, aliondoka patupu, mwenzake hakuonekana katokomea wapi.

Ilimlazimu mwanamuziki, Shaaban Dede kutunga wimbo aliouita, 'Shangwe ya Harusi', akiwa na bendi ya Bima Lee. Baadhi ya mashairi wake ni haya.

"Penzi limegauka majonzi, niliyetaka muoa, kanisaliti, shangwe ya harusi imekuwa kitendawili. Kinamama waliokuwa chumbani kwa bi harusi, wakiimba kwa shangwe, wakijimwayamwaya, kwa furaha, kumpokea mume.

Penzi la simanzi limepasuka hadharani, nilipoingia ndani nisimkute Salma, tausi wangu miye, katoweka."

Wanamuziki hutunga nyimbo zenye matukio halisi yanayotokea kwenye jamii, hii inaonekana kuwa matukio haya yapo, lakini mpaka sasa sababu halisi kwa nini yanatokea haijulikani.

Labda ufanyike uchunguzi kubaini nini hasa huwa kinawasibu.

Mwimbaji, Jerry Nashon 'Dudumizi' akiwa na bendi ya Vijana Jazz, naye alitunga wimbo uliotwao 'Tereza', unaozungumzi maswahibu hayo hayo. Baadhi ya mashairi ya wimbo huo aliimba hivi.

"Aibu, aibu, aibu, umenipa aaa mama, ulinikataa siku ya harusi, mbele ya kasisi bibi, ukanikimbia mbele ya wazazi na rafiki zangu Tereza. Nasema kwa heri kwa uchungu, moyo wangu, unawaka aaa mama..."

Tatizo ni lile lile. Mtu anakwenda hadi kwa wachungaji, lakini anakataa katakata kuwa amekubali kuolewa.

Mbaraka Mwinshehe Mwaruka, akiwa na Super Volcano, alitunga wimbo,' Harusi Imevunjika.' Harusi imepangwa, michango kila kitu, kabla haijafungwa, bi harusi katorokea nchini Gabon, akimwacha bwana harusi alalamika.

"Kweli nimepata niliyoyasikia, sikudanganywa ooo, kumbe uko Gabon, umeshaolewa na mtu mwingine. Masema nasikitika kwani ulichokifanya ni cha dhuluma ooh, wazimu si wazimu huku nimebaki nalia moyoni, sasa ufanye hima uwatumie barua wazazi wako oooh, warudishe mahali yangu ili nipate tafuta mchumba mwingine."

Hii ndiyo dunia, haijawahi kuishiwa maajabu na vituko.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanaume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo, Dar es Salaam, ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. milioni 15 ili wamwachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili, ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

# Nyuma ya Pazia-3

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Siku yake ya mkononi ilitia. Aliingiza mkono mfukoni na kuangalia ni nani anapiga. Hakumjua kwani haikuseviwa. Ina maana namba ilikuwa ngeni. Wasiwasi ukamjia. Akabonyeza kitufe cha kufungulia sauti huku mikono ikiwa inatetemeka. "Ni nini? Ni nani huyu? Macaire amepatikana au..." Akawa anajiuliza maswali, jasho lilikuwa linamtoka na nguvu zikamwisha. Akaamua kukaa kwenye kochi, kwani mwazo alikuwa amesimama.

"Nadhani wewe ndiyo Macky Macaire." "Ndi Ndi Ndiyo mimi." Akajibu kwa woga na sauti ya kutetemeka.

"Vipi mbona hujiamini?" Sauti nzito iliyotulia ilimuuliza baada ya kugundua mpokeaji alikuwa ana kitete.


Macky alishindwa ajibu vipi. Akabaki kimya. Lakini hapo hapo akili ikamjia, akamuuliza aliyempigia.

"Kwani wewe nani mwenzangu?" Badala ya kujibu kikafutia kicheko kifupi cha dharau. "Huna haja ya kujua jina langu na wala haitokusaidia chochote kwa sasa." Ilijibu sauti hiyo kwenye simu kwa kujiamini.

"Tusipoteze sana muda, lengo la kukupigia ni kukutaarifu kuwa mtoto wake Macaire Macky tunaye sisi. Yupo salama salimini na unaweza kuongea naye ukitaka. Ila uhai wake unaweza ukatamatika baada ya wiki moja. Ili tusimuue, unapaswa utoe shilingi milioni 15, utampata akiwa hai bila hata mikwaruzo." Ilikuwa ni habari mpya kwa Macky. Kwanza alichofurahi ni kusikia mtoto wake yu hai, licha ya kwamba hajamsikia sauti. Ila kilichomwacha hoi ni kutakiwa atoe kiasi hicho cha pesa ambacho ni kingi sana kwake.

"Mbona pesa hiyo ni nyingi sana, naomba mnipunguzie..." "Hivi wewe una akili kweli? Badala ya kushukuru tumekutunzia mtoto wako mpaka leo yuko hai, unaomba tupunguze. Sisi tunajua hali yako kiuchumi si nzuri, ndiyo maana tumekwambia kiasi hicho, ungekuwa na pesa wewe tungekwambia utoe shilingi milioni 200, lakini wewe 15 tu zinatosha, tunazitaka hizo kwa muda wa siku saba kuanzia sasa, vinginevyo tutakutaarifu tu sehemu ya kwenda kuchukua maiti ya mtoto wako."Ilisema sauti hiyo ilimtisha mno Macky kutokana na kuonekana haina hata chembe ya huruma.

"Sa sawa nimewaelewa..." "Siyo umetuelewa, tunaitaka hiyo pesa ndani ya siku saba. Na ili kukuthibitishia kuwa mtoto tunaye sisi hebu msikie." "Baba baba..." Ilisikika sauti ya mtoto, halafu ghafla simu ikakatwa.




**"Bwana Macky, nadhani umemka salama." Ni sauti ambayo anaifahamu. Ni ile ile iliyompigia kumfahamisha kumshikilia mtoto wake. Alikuwa ametumia namba nyingine. Hakushangaa sana kwani hizi ni mbinu ambazo hutumiwa na wahalifu. Wana tabia ya kutotaka kuacha alama au ushahidi pale wanapofanya tukio, au uhalifu.**

Macky alijua sauti ya mtoto wake vyema na kuthibitisha ni yeye. Alijua kabisa kuwa wakati Macaire anapewa simu alijua anazungumza na baba yake na ndiyo maana akaanza kumwita. Hata hivyo kabla hajasema lolote simu ikakatwa ghafla. "Kwa nini imekatwa ghafla kabla sijaongea na mwanangu?" Akajiuliza mwenyewe. Ghafla simu yake ikaanza kulia tena. Ilikuwa bado mkononi na akatazama, namba ilikuwa ni ile ile.

"Nadhani umesikia sauti ya mwanao, si ndiyo?" "Mmemkatisha lakini." "Ndiyo, lengo ili kufahamu sauti yake tu na siyo kuzungumza naye. Ili uzungumze naye, fanya ufanyavyo, kakope, kanyang'anye, siku ya saba kutoka leo tunataka mzigo wetu. Baadaye tutakupigia ili kukupa maelekezo ya kufanya ili kuupata mzigo wetu, wapi na saa ngapi." Sauti iliongea na simu ikakatwa.

Macky alibaki kimya. Aliona kama ndoto. Zamani akiwa mtoto na baadaye kijana alikuwa akiziona filamu za aina hiyo kwenye sinema, juu ya watu wanaoteka watoto wa kuhitaji kiasi cha pesa. Leo yamemfika yeye. Mtoto wake ametekwa na watekaji wanataka pesa. Wazo lilimjia ampigie mwalimu Kisanga. Akafanya hivyo na kumtaarifu kuwa mtoto yupo hai, lakini ametekwa huku waliofanya hivyo wakitaka kiasi cha pesa taslimu, Sh. milioni 15.

**********************************

Asubuhi na mapema aliamshwa na milio mkali wa simu. Macky, aliamka kivivu na kuichukua simu yake ya mkononi. Alishangaa kuona namba ni nyingine. Siyo ile aliyopigiwa jana. Kwa maana hiyo alijua siyo wale waliomteka mtoto ni mtu mwingine anapiga.

"Bwana Macky, nadhani umemka salama." Ni sauti ambayo anaifahamu. Ni ile ile iliyompigia kumfahamisha kumshikilia mtoto wake. Alikuwa ametumia namba nyingine. Hakushangaa sana kwani hizi ni mbinu ambazo hutumiwa na wahalifu. Wana tabia ya kutotaka kuacha alama au ushahidi pale wanapofanya tukio, au uhalifu.

"Ndiyo!" Akajibu huku akitega sikio vizuri kwani alijua kuna maagizo mazito yatakuja.

"Ni hivi. Hizo pesa Sh. milioni 15 tunazitaka baada ya siku saba. Tumeongeza siku moja. Ile jana tulikwambia saba leo ingekuwa sita. Lakini tutaanza kuhesabu siku saba kuanzia leo. Kwa maana hiyo, sikiliza kwa makini.

Hizo pesa zinatakiwa uzipeleka kwenye bonde la Kinondoni Mkwajuni, kama unaelekea Magomeni Makaya. Umenisikia vizuri?" "Wapi?" Akauliza tena Macky. "Unapafahamu Kinondoni Mkwajuni kituoni kama unatoka Mwananyamala, Makumbusho, au Kinondoni Morocco?" "Ndiyo napafahamu." Akaitikia. Sasa kama ukitoka hapo kuelekea Magomeni Makanya kabla hujafika si kuna bonde lile la Mkwajuni?" "Nalifahamu." Upande wa kushoto kama unaelekea huko ukipita daraja kuna miti mingi na mteremko mkali, nyumba zinaonekana zipo chini pamoja na miti!" "Ndiyo." "Na eneo hilo kama unatoka Kariakoo, au Kigogo, ukipita kwenye kituo cha Magomeni Kanisani, ukianza kuteremka bonde linakuwa linakuwa upande wako wa kulia, si ndiyo?" "Ndiyo."

"Basi lile eneo ndiyo tunataka utuwekee mzigo wetu pale, ulete kwenye kiroba, mkoba, sanduku, au shangazi kaja hiyo juu yako, sisi tunachotaka kiasi hicho cha pesa." "Kuna njia ya kuteremka kule?" Macky akauliza.

"Ndiyo, ukija mpaka pale kuna njia inashuka kule chini, kuna bonde kali, shuka taratibu utakutana na njia nyembamba na miti mingi na nyumba chache, utashuka hadi sehemu ambayo ni tambarare. Utakata kulia na hatua chache tu utakutana na mti mnene zaidi kuliko yote iliyokuwa hapo. Chini ya mti ndipo utakapoacha mzigo. Cha kukukumbusha ni kwamba usimtume mtu yeyote. Changisheni wanandugu, mkope, mnyang'anye , lakini wewe ndiyo ulete kwa mguu wako. Nadhani umeelewa!" "Ndiyo nimeelewa." "Onyo nimesema uje peke yako na usijaribu ujanja wowote ule, usiwaambie askari polisi siku ya kuleta mzigo iwe siri yako. Kumbuka sisi tuna macho makali, masikio mapana, na mkono mrefu, ukiwaeleza polisi siku ya kuleta mzigo tutajua na inaweza kuwa hatari kwa mwanao." "Nimesikia." "Muda wa kuleta ni kuanzia saa tano usiku mpaka saa sita, na sisi ndiyo tutakuwa tunakupigia simu kukuuliza lini unaleta, wewe huwezi kutupigia kwa sababu hujui namba zetu. Kila siku tunatumia namba mpya na tutakayokupigia hatuitumii tena kwa ajili ya usalama wetu. Ujanja wowote utakuwa ni mauti kwa mwanao na kwako pia." Ilimaliza simu ile na kukatwa.

*Itaendelea Jumapili*



# RAIS SAMIA, WASANII WAMLILIA DIDA

WATU mbalimbali mashuhuri nchini, wakiogozwa na Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, wameendelea kutoa salamu zao za rambirambi, wakionekana kushtushwa na kifo cha ghalfa cha mtangazaji, mjasiriamali na MC maarufu nchini, Khadija Shaibu maarufu kama Dida.

Mtangazaji huyo alifariki usiku wa juzi kuamkia jana kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili alipokuwa amelazwa baada ya kuugua kwa muda mfupi.

Katika salamu zake alizotoa jana, Rais alitoa pole kwa ndugu, jamaa, marafiki na wafanyakazi akiwataka wawe na subira.

"Ninatoa salamu za pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na wafanyakazi wa Wasafi Media Group kwa kuondokewa na ndugu yetu, Khadija Shaibu (Dida). Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma awape subra.

Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwa hakika kwake yeye tutarejea," aliandika Rais Samia kwenye mtandao wake wa instagram.

Wasanii, watangazaji na wanamitindo mbalimbali nao wameendelea kumimina salamu zao za rambirambi wakionekana kuguswa na msiba huo.

Mwigizaji Wema Sepetu aliandika maneno haya. "Ngumu kuamini. Ni maumivu. Tutakukumbuka kwani ulikuwa kipenzi cha wengi. Pumzika kwa amani da Didah wangu. Daaaah jamani."

Mwigizaji mwingine Shilole, yeye aliandika hivi. "Nimepokea kwa masikitiko makubwa kifo cha Dada yangu Dida. Kifo ni ukumbusho tosha kwa sisi tuliobaki, Kila nafsi itaonja umauti."

"Ayubu 14:1. Mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke siku zake za kuishi si nyingi, naye hujaa tabu." Huyu ni mwigizaji Irene Uwoya, aliyenukuu kifungu hiki ndani ya Biblia Takatifu.

Msanii wa Bongo Fleva, Zuchu, aliandika maneno yafuatayo. "Sisi sote marejeo yetu ni kwako. Basi tunaomba utuchukue kipindi uko radhi nasi. Yah Rabbi mpe dada yetu kauli na umsamehe mapungufu yake hakika sisi sio wakamilifu, ukamilifu ni wa kwako pekee."

Nandy naye hakuficha maumivu yake kufuatia msiba huo. "Dada Dida, Mungu akupe pumziko jema, poleni ndugu, jamaa na marafiki." Alizikwa jana makaburi ya Kisutu, jijini Dar es Salaam.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TUCHEL ATAJWA MAN

KLABU ya Manchester United itafufua mazungumzo na kocha wa zamani wa Chelsea, Thomas Tuchel iwapo watamfukuza kazi Erik Ten Hag. ***(ipaper)***

### MABOSI MAN KUAMUA

UONGOZI wa Manchester United utakutana Jumanne kujadili masaibu ya klabu hiyo baada ya mmiliki mwenza Sir Jim Ratcliffe kuwatazama wakicheza na Aston Villa kwenye Ligi Kuu England leo Jumapili. ***(Athletic)***

### INZAGHI AMEKATAA

KOCHA wa Inter Milan, Simone Inzaghi, amekataa ofa ya kumrithi Erik Ten Hag kule Old Trafford ***(Sportitalia)***

### MEULENSTEEN KUREJEA

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Rene Meulensteen amesema atakuwa tayari kurejea ikiwa Ruud van Nistelrooy, kocha msaidizi kwa sasa katika klabu hiyo, atakuwa kocha mkuu. ***(No Tippy Tappy Football Podcast, via Mirror)***

### DURAN AFUATILIWA

REAL Madrid inamfuatilia kwa karibu mshambuliaji wa Aston Villa na Colombia, Jhon Duran mwenye umri wa miaka 20. ***(Football Insider)***

### PRADAS AIVUTIA ARSENAL

ARSENAL inavutiwa na mshambuliaji wa Barcelona mwenye umri wa chini ya miaka 19 wa Barcelona, Arnau Pradas. ***(Mundo Deportivo)***

### WHARTON KUMRITHI RODRI

KLABU ya Manchester City imemjadili kiungo wa kati wa Crystal Palace na England, Adam Wharton mwenye umri wa miaka 20, kama kiungo mbadala wa Rodri ambaye ni majeruhi. ***(Football Insider)***

### CALVERT-LEWIN AWANIWA

EVERTON itajaribu kufufua mazungumzo ya mkataba mpya na mshambuliaji wa England, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 27, ikiwa mapendekezo ya kutwaa umiliki wa Friedkin Group yatakubaliwa. ***(ipaper)***

### EZE NA LIVERPOOL

LIVERPOOL ina nia ya kumsajili fowadi wa England, Eberechi Eze mwenye umri wa miaka 26 kutoka Crystal Palace. ***(Football Insider)***

### PARTEY AWINDWA

BARCELONA na Atletico Madrid zote zinapanga kumnunua kiungo wa kati wa Arsenal na Ghana, Thomas Partey mwenye umri wa miaka 31. ***(Fichajes, via TeamTalk)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RATCLIFFE AJITOA KUHUSU TEN HAG

●●●Asema yeye hahusiki na uamuzi wa mwisho kama...

**MANCHESTER, England**

MMILIKI mwenza wa Manchester United, Sir Jim Ratcliffe amekiri kuwa hahusiki na uamuzi wa mwisho kuhusu mustakabali wa kocha Erik ten Hag.

Ten Hag yuko kwenye presha kubwa baada ya kuanza vibaya msimu huu, huku mashabiki wengi wakitaka Mholanzi huyo afukuzwe baada ya kuiongoza timu hiyo kwa kushinda mara tatu pekee katika mechi kumi zilizopita.

Alipoulizwa na BBC Sport kama bado ana imani na Ten Hag, Ratcliffe alijibu: "Sitaki kujibu swali hilo.

"Nampenda Erik. Nadhani ni kocha mzuri sana lakini mwisho wa siku sio jukumu langu, ni timu ya usimamizi inayoendesha Manchester United ambayo inapaswa kuamua jinsi tunavyoendesha timu vizuri katika mambo mengi tofauti.

"Lakini timu hiyo inayokimbiza Manchester United imekuwa pamoja tu tangu Juni au Julai. Hawakuwapo Januari, Februari, Machi au Aprili - Omar Berrada na Dan Ashworth walifika tu Julai.

"Wamekuwapo tu, unaweza kuhesabu ndani ya wiki karibu. Hawajafika kwa muda mrefu kwa hiyo wanahitaji kujitathmini na kufanya maamuzi ya busara.

"Lengo letu liko wazi sana: Tunataka kuirejesha Manchester United pale inapopaswa kuwa, na bado haijafika, ni wazi. Hilo liko wazi sana."

Makocha kama Graham Potter, Thomas Tuchel, Eddie Howe, Massimiliano Allegri na Gareth Southgate wote wametajwa kuwa warithi wa Ten Hag, ambaye alisaini mkataba mpya wa miaka miwili Julai baada ya United kuamua kumbakisha.

# SLOT ATAFUTA NAFASI KWA DARWIN NUNEZ

**LIVERPOOL, England**

ARNE Slot amefunguka kuhusu changamoto ya kutafuta njia bora ya kumtumia Darwin Nunez, huku fowadi huyo akihangaika kupata nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha Liverpool.

Nunez amejumuishwa katika michezo saba ya Wekundu hao hadi sasa katika kampeni ya 2024/25, akicheza mechi nne kwenye Ligi Kuu England, tatu kati yake akitokea benchi.

Wakati Diogo Jota anaonekana kuwa straika chaguo la kwanza la Slot, Nunez ametatizika kuweka alama yake kwenye kikosi.

Nafasi kwenye winga ya kushoto inasalia kuwa chaguo kwa Nunez, lakini Luis Diaz yuko na Cody Gakpo amevutia kama msaidizi wake, na kumwacha mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay nje ya mipaka.

Slot amekiri kwamba kujua nafasi ya Nunez katika kikosi chake bado ni mradi unaoendelea kwa Liverpool, ambao wana nia ya kumwona nyota huyo akipata muda zaidi uwanjani.

"Nadhani ni changamoto kwetu viongozi na tunapaswa kuleta ubora," alisema akiwaambia waandishi wa habari.


"Tunajaribu kutafuta njia tofauti za kumweka Darwin kuliko Diogo kwa sababu sio wachezaji sawa.

"Wachezaji wenzao pia wanazoeana na mchezaji wanayecheza naye. Hilo pia ndilo jambo ambalo mimi kama kocha natakiwa kufanya.

"Ndiyo, hakufunga katika mchezo wake wa mwisho kwa sababu alikuwa ameotea pia. Mletee nafasi, ana uwezo wa kufunga lakini kwa bahati mbaya hatukuweza kumleta kiasi hicho katika nafasi tunayotaka.

"Kama niwe mkweli kabisa hata Diogo hakuwa na mabao mengi. Nafikiri mabao mengi tunayofunga yanatokana na mawinga wetu hadi sasa na Diogo alifunga mawili tulipocheza na West Ham wakati akicheza kutoka namba 10."

Liverpool watarejea uwanjani Jumamosi watakapomenyana na Crystal Palace katika Uwanja wa Selhurst Park katika mechi ya Ligi Kuu ya Uingereza kabla ya mapumziko ya kimataifa.



# Barca yatoa ofa ya mkataba mpya kwa de Jong

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA imemwonya kiungo Frenkie de Jong kwamba ni lazima akubali masharti ya mkataba mpya kabla ya dirisha la usajili la Januari ikiwa anataka kusalia katika klabu hiyo, ripoti imedai.

Mustakabali wa De Jong katika klabu ya Barcelona kwa muda mrefu umekuwa na uvumi mkubwa na hali ya sintofahamu imeongezeka baada ya Mholanzi huyo kuingia miaka miwili ya mwisho ya mkataba wake unaotarajiwa kumalizika 2026.

Kulingana na Sport, kuna nia kutoka kwa kila mtu anayehusika kutatua nyongeza, lakini masharti ya makubaliano yoyote mapya hadi sasa yameonekana kuwa magumu.

De Jong anadaiwa kiasi kikubwa cha mshahara aliokubali kuahirisha wakati wa janga la COVID-19, kabla ya kukubali kucheleweshwa zaidi kusaidia klabu kusawazisha hali yao ngumu ya kifedha.




Barcelona wamejaribu kufikia makubaliano juu ya mishahara hiyo katika mazungumzo ya hivi karibuni ya mkataba, lakini maendeleo yanasemekana kukwama.

Barcelona wanazidi kuwa na wasiwasi juu ya uwezekano wa kumpoteza De Jong kwa uhamisho wa bila malipo, huku Chelsea, Manchester United, Bayern Munich na Paris Saint-Germain zote zimeonesha nia ya kutaka huduma yake.

Barcelona inasemekana kumuonya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kwamba ana miezi mitatu kukubaliana na masharti ya kuongeza muda kabla ya klabu kuanza kupanga maisha bila yeye.

De Jong amekataa mara kwa mara kuondoka Barcelona na amekiri hadharani kuchanganyikiwa kwake kwa kile anachoamini ni majaribio ya kumtaka aondoke katika klabu hiyo.

# Rudiger amtaka Saliba Madrid

**MADRID, Hispania**

MLINZI wa kati wa Real Madrid, Antonio Rudiger amekiri nia yake ya kutaka kucheza pamoja na William Saliba katika dimba la Santiago Bernabeu.

Saliba amefurahia miaka kadhaa katika safu ya ulinzi ya Arsenal na kujikuta akihusishwa na vigogo wa Ulaya Madrid na Paris Saint-Germain, ambao wote wanatarajiwa kuwa sokoni kutafuta beki mpya siku za usoni.

Alipoulizwa ni nani atamsajili kucheza naye katika ubia wa beki wa kati katika ndoto, Rudiger aliliambia gazeti la The Inside Scoop: "Saliba.

"Nimefurahishwa na mlinzi wangu wa kati, Eder Militao, kwa sababu pia ana uwezo, ana nguvu sana, anarejea katika ubora wake baada ya jeraha kubwa, lakini kuna michezo mingi na lazima uzunguke, kwa hiyo kuwa na Saliba itakuwa nzuri.

"Kama ataendelea kufanya kile anachofanya... sijaribu kuwatisha mashabiki wa Arsenal lakini, mwisho wa siku, ni wazi kwamba akifanya anachofanya..."

Rudiger aliendelea kumtaja Saliba kama mmoja wa mabeki watatu bora wa kati duniani pamoja na mchezaji mwenzake wa Arsenal, Gabriel.

"Sitatoa amri," alisisitiza Rudiger.



## HABARI MICHEZO

# NGORONGORO HEROES, KENYA, KUFUNGUA CECAFA LEO

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Tanzania chini ya miaka 20, leo itafungua michuano ya kuwania Kombe la Afrika Mashariki kwa vijana chini ya umri huo, itakapokipiga dhidi ya Kenya, mechi ikichezwa, Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam.

Mchezo huo utafanyika saa 10:00 jioni, huku Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Charles Boniface Mkwasa, akisema kikosi chake kimejiandaa si kwa kushinda mchezo huo tu, bali kulibakisha kombe nyumbani.

"Nimeridhika na maendeleo ya kikosi changu, nadhani vijana wapo tayari, tutafanya vyema kwenye mashindano haya, hata kutwaa ubingwa," alisema Mkwasa.

Mbali na mchezo huo saa 10:00 jioni, majira ya saa 18:00 jioni kutakuwa na mchezo mwingine kati ya Sudan dhidi ya Djibouti, ambao utachezwa, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Shirikisho la Vyama vya Mpira wa Miguu Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), michezo hiyo itaendelea tena kesho, Sudan Kusini itakapokipiga dhidi ya Burundi, Uwanja wa KMC Complex, saa 10:00 jioni na saa 12:00 jioni, Azam Complex, Uganda itakumbana na vijana wa Ethiopia.

Ratiba inaonyesha kuwa michuano hiyo itaendelea tena Jumanne, Tanzania, itakaposhuka kucheza dhidi ya Djibouti, Uwanja wa KMC Complex jioni, na Sudan kukipiga dhidi ya Rwanda, saa 12:00 jioni, Uwanja wa Azam Complex.

Michuano hiyo inayofanyika nchini mwaka huu, imegawanywa kwenye makundi mawili, A, likiwa na Tanzania, Rwanda, Sudan, Kenya na Djibouti, huku kundi B, likiwa na timu za Burundi, Ethiopia, Sudan Kusini na Uganda.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Iboni ya Kondoa mkoani Dodoma, wakicheza mpira katika Uwanja wa Shule hiyo juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kocha wa KVZ haridhishwi na kiwango cha timu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA wa Timu ya KVZ FC, Ali Mohmed Ameir, amesema haridhishwi na matokeo anayoendelea kuyapata kwenye Ligi Kuu Zanzibar.

KVZ FC juzi ilipata sare nne mfululizo baada ya kufungana 1-1 katika mchezo wake wa tano dhidi ya Zimamoto SC, mchezo uliochezwa kwenye dimba la New Amaan Complex.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Ameir alisema kwamba, hakuna mwalimu anayeridhika na matokeo ya sare au kufungwa katika mchezo wanaohitaji alama tatu.

Alisema kikosi chake kimefanikiwa katika kukifanyia maboresho eneo la ulinzi na nafasi ya kati ambapo kumekuwa na muunganiko mzuri.

Alisema bado anakazi kubwa katika kufanyia maboresho eneo la ushambuliaji ili kuzitumia vizuri nafasi ambazo wanazipata.

"Tumefanikiwa kucheza vizuri katika nafasi ya ulinzi, lakini tunahitaji kufanya vizuri zaidi katika nafasi ya ushambuliaji bado hatupo vizuri, tunatengeneza njia na nafasi ya kushinda lakini washambuliaji wanashindwa kufunga," alisema.

## Fadlu: Hatuna wa kumlaumu

INATOKA UK. 24

ma Simba waliingia kwenye mtego, ndiyo maana walifanikiwa kurudisha mabao yote mawili na ingewezekana wangeweza kupata hata la tatu.

"Kikubwa ni kwamba tuliwaheshimu hasa kipindi cha kwanza, sasa wakaingia kwenye mtego kudhani tutakuja hivyo hivyo kipindi cha pili. Matokeo yake tulibadilika na kushambulia, mabao yote ni ya kushtukiza, wao walijua sisi tutakuwa tunakaba tu muda wote kama ilivyokuwa kipindi cha kwanza," alisema kocha huyo ambaye alikuwa beki wa kushoto wa zamani wa timu hiyo.

Mabao ya kipindi cha pili ya Hassan Abdallah na Ernest Malonga, yaliiwezesha Coastal Union kurudisha mabao yote mawili waliyofungwa kipindi cha kwanza na Mohamed Hussein 'Tshabalala', na Leonel Ateba na kuifanya mechi hiyo iliyochezwa juzi, Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam kumalizika kwa sare ya mabao 2-2 na kuwashangaza wanachama na mashabiki wa Simba waliokuwa uwanja ni hapo na waliokuwa wakiangalia kwenye televisheni.

Sare hiyo inaifanya Simba kupanda hadi nafasi ya pili ikifikisha pointi 13 kama Fountain Gate na kuishusha kwenye nafasi hiyo kutokana na kuwa na uwiano mzuri wa mabao ya kufunga na kufungwa.

Pamoja na sare hiyo, bado Coastal Union inasalia nafasi ya 13 ikifikisha pointi tano, ikiwa ni sare ya pili kwenye Ligi Kuu.

## Gamondi aiendea chimbo Simba

INATOKA UK. 24

sisi tutajiandaa vuzuri zaidi ili kupata ushindi," alisema. Mchezo huo utachezwa miezi miwili tu baada ya mchezo uliopita kati ya watani hao wa jadi uliopigwa, Agosti 8, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Yanga ikishinda bao 1-0, lililofungwa na Mkongomani Maxi Nzengeli, katika mchezo wa nusu fainali ya Ngao ya Jamii, wiki moja kabla ya kuanza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Utakuwa pia ni mchezo wa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ambapo Yanga itataka kuendeleza ubabe wake, baada ya kushinda mechi zote mbili za ligi msimu uliopita.

Katika mchezo wa mzunguko wa kwanza, Yanga iliichakaza Simba mabao 5-1, mechi ikipigwa Novemba 5, 2023, na mzunguko wa pili, ikashinda tena mabao 2-1, mechi ikichezwa Aprili 20 mwaka huu.

Kwa sasa inashika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikishinda michezo yote minne iliyocheza, ikikusanya pointi 12, mabao manane na haijaruhusu wavu wake kuguswa.

Michezo

Jumapili Oktoba 6, 2024

Nipashe



## Ratcliffe ajitoa kuhusu Ten Hag

UKURASA 21

# Gamondi aiendea chimbo Simba

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema muda wa wiki mbili uliosalia unatosha kabisa kuwasoma na kuwaangalia wapinzani wake Simba, kabla ya kupanga mikakati kwa wachezaji wake kukabiliana nao, Oktoba 19, mwaka huu, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Gamondi, alisema pamoja na kwamba hufanya maandalizi katika kila mchezo, lakini unaofuata ni wa dabi na anataka kuwapa furaha mashabiki wa timu hiyo ambayo siku zote wako nyuma yao kuwasapoti.

"Nadhani sasa wanachama na mashabiki wa Yanga wamerejesha furaha yao baada ya ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Pamba, sasa tunakwenda kucheza na Simba, ni muda mrefu bado, ni kama wiki mbili mbele, tutajiandaa kikamilifu, sisi tunajiandaa kwa michezo yote, lakini hii ni dabi, ni muda sasa wa kukaa na kuwasoma taratibu na kuwawekea mikakati ya kukabiliana nao, huu utakuwa mchezo mzuri na zawadi kwa ajili ya mashabiki wetu ambao wamekuwa bega kwa bega na sisi kutusapoti kila tunapokwenda," alisema kocha huyo raia wa Argentina.

Alikiri kuwa hautokuwa mchezo rahisi kwani siku zote dabi haijawahi kuwa rahisi, lakini akifurahi zaidi kucheza Uwanja wa Benjamin Mkapa, ambao unaruhusu aina yoyote ya mfumo ambao kocha anauhitaji.

"Nadhani tutacheza Uwanja wa Benjamin Mkapa, utakuwa mchezo mzuri, utakuwa mgumu, lakini tuna furaha kucheza mchezo huo, kila timu itacheza vizuri kutokana na aina ya uwanja, kwa maana hiyo kwetu

INAENDELEA UK 23



Beki wa Simba, Shomari Kapombe akiwania mpira na wachezaji wa Coastal Union, katika mchezo wa Ligi Kuu uliopigwa Uwanja wa KMC Mwenge Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# FADLU: HATUNA WA KUMLAUMU

## ●●●Asema kwa sasa ana kazi ya kubadili mitazamo na...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya sare ya kushangaza dhidi ya Coastal Union, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema hawana wa kumlaumu katika mchezo huo, huku akisema ana kazi ya kufanya ili kubadili mitazamo ya wachezaji wake.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu hiyo dhidi ya Coastal Union, ikiisha kwa mabao 2-2, Fadlu, alisema wachezaji wake walicheza kwa kuridhika na kuichukulia poa mechi hiyo.

Maxi Nzengeli

Alisema wachezaji wake walitakiwa waimalize mechi hiyo kipindi cha kwanza kwani walikuwa na uwezo wa kufunga zaidi ya mabao mawili, lakini hawakufanya hivyo, badala yake wakaonekana kama wameimaliza mechi kabla ya mabao mawili ya kushtukiza yaliyoonekana kuwachanganya.

"Mechi ilitakiwa kumalizwa kipindi cha kwanza kwa kufunga goli la tatu, lakini kwa kilichotokea nina kazi ya kubadili mitazamo ya wachezaji, tutarudi uwanja wa mazoezi kujiandaa kuelekea mchezo ujao dhidi ya Yanga," alisema kocha huyo.

Hata hivyo alisema ana kazi kubwa kuelekea mchezo huo wa Oktoba 19, kwani wachezaji wengi wanakwenda kwenye vikosi vya timu za taifa, hivyo atabaki na baadhi ya wachezaji tu.

"Hakuna la kufanya, tutaendelea na mazoezi na hawa waliopo kuelekea kwenye mchezo huo muhimu," alisema Fadlu.

Kwa upande wa Kaimu Kocha Mkuu wa Coastal Union, Joseph Lazaro, alise-

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >